# Kitabu ndogo kuhusu utetea ukristo kwa wachungaji na wafanya kazi ya kikristo

**Jaribu** mbele **uamini**!

1 Watesalonika 5:21–22

AC/FAR
Africa Centre for Apologetics Research

Kumbuka hizi hatua tatu:

**Jaribu** kila kitu

**Shika** lililo nzuri

**Jiepushe** na aina yote ya ubaya

# Kuhusu The Africa Centre for Apologetics Research (ACFAR)

Kazi ya ACFAR imesimamishwa juu ya « amri kubwa » ya Yesu katika Matayo 28 wapi ametumuru kufanya mataifa kuwa wanafunzi. Kufanya wanafunzi kwa njia ya Biblia inahitaji kufikisha waamini kukomea kiroho na katika umoja. Na kwa hiyo, inabidi tufuate mufano ya mitume.

Africa Centre AC|FAR for Apologetics Research

## Tunasimamia mambo matatu:

Kwanza, tumepewa kazi ya kutayarisha watu wa Mungu ***kutambua***—hii ni kuwasaidia kutoautisha kupitia maandiko katikati ya ukweli na uwongo, uzuri na ubaya, giza na nuru-na mara nyngi, katika masemo ya Charles Spurgeon, kujua tofauti kubwa « kati ya ukweli na *kila mara* ukweli » inayotumiwa mara nyingi na mazehebu na manabii ya uwongo. Wale wanaofundisha mafundisho ya uwongo ya kiroho ya uwongo wanaweza kwa pahali hakuna « chakula kigumu ni kwa watu wazima, walio na akili zao, kwa kutumiwa, zimekwisha kuzobelea kufahamu mema na mabaya » (Waebrania 5:14).



Pili, tunatafuta kufundisha waamini kwa ***ulinzi ya imani*** « waliopewa watakatifu mara moja tu » (Yuda 3–4). Amri hii inatulazimisha « kuipigania kwa nguvu » imani hii mbele ya upinzani—hapana na silaha za kibinadamu ya kuangamiza kwa uwongi, lakini kwa njia rahisi nay a akili, kwa ukweli na juhudi, tukizungumuza kwa unyenyekevu ukweli Mungu aliotofunulia kwa njia ya Roho yake ndani ya Maandiko Matakatifu. Tito 1 inalazimisha wachungaji—wanaokuwa kwa mustari ya kwanza kwa kupiga uongo—kushika « nenno la imani kama alivyofundishwa aweze kuonya watu kwa mafundisho ya kweli na kuwashinda wenye kubishana naye. »

Tatu, tunatafuta kuamusha wakristo kwa kazi iliyozarauliwa lakini ya maana sana, ndio ***kuhubiri habari ya mazehebu***. Hii inamaanisha kusaidia kwa huruma wanaume, wanawake na watoto walioshikwa katika mutego ya vikundi ya mafundisho ya uongo kujua Yesu Kristo kama Mungu wa kweli anayeishi na kukusanya tumaini ile Yesu peke yake anaweza kuwapa!

**Leo wakristo wameviziwa na mazebehu na waalimu wa uongo wanaotafuta kudanganya, kupoteza na kuharibu imani yao.** Waamini wengi—hata wachungaji—hawajatayarishwa kupigana na hii. ACFAR inafundisha wachungaji na wafanya kazi wengine ya kikristo kufahamu na kutumia ukweli ya Biblia ili wajibu ginsi inavyofaa kwa machanganyiko ya kiroho na upinzani zinazotuzingira.



Kwa neema ya Mungu, tunafutilia kazi hii kupitia utafuti juu ya vikundi ya mazehebu, kupitia radio na kuchapisha na kugawa habari ya kusaidia, kwani kuna njaa sana kupata majibu. Na hii, inawezekana kwa njia ya kushiriki na makanisa wanaojitoa kwa kweli, utumishi zinazokuwa na nia sawa na watu waaminifu.

Tunatumaini ya kwamba utaomba pamoja nasi na kutuunga mukono tukitafuta sana kutimiza mwito ya Amri Kubwa ya kufanya wanafunzi, tukikomalisha hapana tu waamini, lakini wakristo wale wanaweza kujaribu kila kitu, ginsi inavyosemwa: « Lakini jaribuni mambo yote; shikeni lililo njema; mujitenge na ubaya wa kila namna » (1 Watesalonika 5:21–22).

# Kutetea imani (apologétique) na wewe

Neno *apologétique inatoka kwa neno la Kigriki apologia* (kupigania). Apologétique—ikielekea kupigania ukristo—inaonekana kuwa kama ufundi ndani ya kanisa ya sasa. Leo, hii inaonekana kuwa kama hivi: « Mungu ni Mungu wa mapendo. Kwa hivi tupendane. Hatungeuliza kuhusu imani ya wengine, kwa sababu hii ni kukosa mapendo. » Mbali na mafikili hii ya kupoteza, Yesu—mapendo iliyochukua mwili—mara kwa mara alipinga (mara ingine na nguvu yote) imani ile alikutana naye (ona Matayo 23). Tunapashafuata mufano wake.



> Apologétique
> ἀπολογία
> inaonyesha kwa sababu gani tunaamini ile tunaamini.

Maandiko yanatupatia mufano ya kufuata katika apologétique. Mutume Paulo, kwa mufano, alitenda kama mwenye kupigania imani ndani ya Kristo wakati alipotoa sababu ya imani kwa Wayuda na mataifa (Matendo 17:15–34; 18:34). Apolo ni mufano ingine kubwa, kwa sababu kwa Akaya alipigania sana imani, akihamakia wasioamini katika mabishano ya wazi na kuhakikisha kutoka maandiko ya kwamba Yesu ni Kristo (Matendo 18:24–28).

Apologétique inaleta uhakika ya kweli inayoleta nguvu kwa wasioamini kuchagua ukristo kuliko dini ingine yeyote. Apologétique inawezakutumiwa kuonyesha kwa musioamini ya kwamba njia zingine zote kwa « meza ya karamu » ya dini za dunia si njia za kweli kabisa kwa sababu ni za uwongo. Apologétique inaweza kuondoa ile inayofunga mafikili ya wasioamini kujibu kwa Habari Njema.

Apologétique haileti tu kupigania imani, lakini inaleta pya usalama kwa wakristo. Waamini wanaweza kuwa na uhakika ya kwamba imani yao si kipofu katika giza, lakini uamuzi ya akili inayosimamia ukweli. Apologétique haibadilishi imani yetu; inasimamisha imani yetu.

Ron Rhodes • *5-Minute Apologetics for Today* (Harvest House, 2010)






AC|FAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Dini zote si sawasawa

Watu wengine wanasema ya kwamba dini zote ni sawasawa kwa musingi na zinakuwa tu na tofauti ya kidogo sana. Ukweli ni ya kwamba dini zote ni *tofauti* kwa musingi na zinafanana tu juu juu.

Wengine wanasema dini zote ni sawasawa kwa sababu zote zinafundisha namna ya kuishi (*éthique*). Ukweli ni ya kwamba dini zingine zinatafuta kusaidia watu wabaya kuwa wazuri wakichagua njia muzuri ya upeke kwa kuishi. Ukristo, kwa upande mwingine, unaalika watu wale wamekufa kiroho kukuwa hai kiroho (Yoane 3:5).



Hii inatimilika tu kupitia zabihu ya kifo ya Yesu (2 Wakorinto 5:21). Yesu alisema ya kwamba ile aliyosema ni juu ya mafundisho ya watu wengine wote. Alisema ya kwamba umutu wake ulihusika tu na wokovu (Yoane 14:6). Wale waliomufuata walihakikisha hii (Matendo 4:12; 1 Timoteo 2:5). Yesu alionya pya kuhusu wale wanaotafuta kuleta Kristo mwengine (Matayo 24:4–5).

> Kujitoa ya mutu kwa mafikili ya kwamba dini zote ni sa wasawa inasimama juu ya kutokujua yake ya dini hizi.

Dini mbalimbali zinafundisha pya maoni mbalimbali kuhusu Mungu. Yesu alifundisha utatu wa Mungu (Matayo 28:19). Muhammad, mwenye alianzisha Islamu, alifundisha ya kwamba Mungu hana utatu. Dini ya Kihindu inahusika na miungu wanaokuwa tu kuendelea ya Brahnam. Budhisme inafundisha ya kwamba mafikili kuhusu Mungu haina maana yoyote. Ikiwa mutu moja ni mwenye haki, wengine ni wawongo. Ikiwa Yesu alikuwa haki, kama waamini wakristo, wengine wote ni wawongo.

Ron Rhodes • *5-Minute Apologetics for Today* (Harvest House, 2010)

# Wakristo *wanawezwa* kudanganywa



Ukweli, sababu na kufikili ya wazi ni muhimu kwa sababu wakristo wanawezwa kudanganywa kwa njia ya mafundisho—inamaanisha, wanaweza kuanguka katika mafundisho ya uwongo.

Ezekieli 34:1–7 inahakikisha wazi ya kwamba kondoo za Mungu wanawezwa kuteswa na kupelekwa mbali na wachungaji wabaya. Zaidi, Yesu alileta angalisho kwa wanafunzi wake kuhusu manabii ya uwongo wanaoweza kuonekana kuwa wazuri toka inje, lakini wanakuwa hatari ndani yao (Matayo 7:15–16). Kwa nini Yesu aliwapa uaangalifu kama hawangewezwa kudanganywa?

Wakristo wale hawana musingi katika ukweli ya Biblia ni rahisi kwao kuanguka katika mafundisho ya uwongo. Kwa hivyo, wakristo wanahitaji kusimama wakati wote na *kila siku* Katika Maandiko.

Yesu aliambia pya wanafunzi wake: « Angalieni musidanganyiwe na mtu. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema: Mimi ndiye Kristo; na watadanganya watu wengi … Na manabii wengi wa uwongo watasimama na kudanganya watu wengi » (Matayo 24:4, 5, 11). Kwa sababu gani Yesu alileta angalisho kwa wanafunzi wake kuhusu kudanganyiwa ikiwa hawangewezwa kudanganywa na kwa mwisho kuamini uwongo?

Vivyo hivyo, katika 2 Wakorinto 11:2–3, mtume Paulo alileta angalisho kwa wakristo wa Korinto kuhusu kuwezekana kupelekwa kando na kujitoa ya kweli kwa Kristo. Paulo aliona wazi ya kwamba inawezekana kwa wakristo kudanganywa na kupelekwa kando na mafundisho ya uwongo.

Katika Matendo 20:28–30, Paulo alitoa angalisho kwa wazee wa Efeso kuchunga sana kundi la Bwana na zaidi sana kukesha kuhusu waalimu wa uwongo, wanaongea « maneno bure, kupeleka mbali wanafunzi nyuma yao » (ona Waefeso 4:14; 2 Timoteo 4:3–4).

Ron Rhodes • *5-Minute Apologetics for Today* (Harvest House, 2010)



Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

AC|FAR
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Manabii na waalimu ya uwongo

Mara nyingi Maandiko yanaleta angalisho kuhusu manabi na waalimu ya uwongo kwa sababu hata watu wa Mungu wanawezwa kudanganywa (Ezekieli 34:1–7; Matayo 7:15–16; 24:4, 11). Kwa hivi, Biblia inaonya waamini *kujaribu* wale wanaojiita kuwa manabi (one 1 Yoane 4:1–3).

**Namna gani waamini wanaweza kutambua nabi ya uwongo? Hapa ni mambo machache ya muhimu:**

- Manabi ya uwongo wanatabiri mambo yale hayawezi kutimilika (Kumbukumbu la Torati 18:21–22).
- Mara ingine manabi ya uwongo wanaongoza watu kufuata miungu ao sanamu (ona Kutoka 20:3–4; Kumbukumbu la Torati 13:1–3).
- Mara nyingi manabi ya uwongo wanakana ukweli ya umungu wa Yesu (Wakolosayi 2:8–9).

Inatupasa kufuata mufano ya watu wa Beroa kwa njia ya kujaribu ukweli yote inayosema ni ya Andiko



(Matendo 17:11; 1 Watesalonika 5:21).

- Mara ingine manabi ya uwongo wanakana umutu wa Yesu (1 Yoane 4:1–2).
- Mara ingine manabi ya uwongo wanasimamia kufuata sheria, kama kujizuiza na vyakula fulanifulani kwa sababu ya kiroho (1 Timoteo 4:3–4).
- Mara nyingi manabi ya uwongo wanatia watu moyo kwa kujitesa (Wakolosayi 2:16–23).
- Mara ingine manabi ya uwongo wanafundisha ya kwamba ndoa ni mbaya (1 Timoteo 4:3).
- Mara nyingi manabi ya uwongo wanaendelesha aina mbalimbali ya ubaya (Yuda 4–7).

Ikiwa anayejiita nabi anasema neno lolote lile linapinga sehemu chochote ya Neno la Mungu, lazima mafundisho yake kutupwa. Neno la Mungu ni chombo chetu ya kupima naye ukweli, inayoonyesha makosa.

Ron Rhodes • *5-Minute Apologetics for Today* (Harvest House, 2010)



# Mafundisho *(doctrines)* ya maana ya imani ya kikristo



Mafundisho ya maana yanaeleza ukristo kwa muda ya miaka 2.000. Wakristo wote wanaotaka kuwa na imani inayosimama juu ya Biblia wanashika namna fulani ya mafundisho yale ya musingi. Wakristo wanaweza kutofautishana namna gani wanatimiza mambo madogomadogo ya imani yao, lakini wanaweza kukubaliana kuhusu mafundisho ya maana—zile kweli za musingi.

**Tunaweza kutambua mambo ya maana ya mafundisho ya imani ya kikristo kwa kuona mafundisho ya musingi ya Habari Njema, iliyo wokovu ya mwanadamu kupitia uzima, kifo na ufufukko ya Yesu Kristo.** Wokovu, ginsi Mungu alivyotufunulia kupitia Maandiko Matakatifu, inaelezwa kama usamehe wa zambi na uzima wa milele pamoja na Mungu kwa njia ya kukiri ya kwamba « Yesu ni Bwana » na kuamini ya kwamba Mungu alimufufua Yesu toka wafu (Waroma 10:9). Tukichunguza ujumbe ya Habari Njema, tunaweza kuona mafundisho 14 ya maana ili wokovu itimilike.

Mafundisho ya maana ya ukristo yanahusu:

- Mungu ni nani
- Yesu Kristo ni nani
- Upendo ya Mungu kwa watu na hamu yake kuwaokoa

*Mafundisho ya maana ya wokovu yanayohitajika kuwa kweli ili mutu yeyote ajue Mungu na kukolewa ni:*

## 1 Umoja wa Mungu

Kuna Mungu moja tu wa kweli. Yeye anakuwa tangu milele hata milele. Kuna Mungu, Muumba mumoja—na mumoja tu—ya ulimwengu.

## 2 Utatu wa Mungu

Mungu ni mumoja, anaishi kwa milele ndani ya Watu tatu: Baba, Mwana na Roho Mutakatifu.

## 3 Kupungukiwa ya mwanadamu

Mungu akiwa na umutu, anataka uhusiano wa peke na wanadamu. « Kupungukiwa ya mutu » inamaanisha ya kwamba kila mutu ametengwa kiroho na Mungu na hana uwezo kamwe ya kujiokoa yeye mwenyewe.



Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

AC|FAR

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

## 4 Kuzaliwa ya Kristo na Bikira

Yesu alizaliwa kwa njia ya mujiza: Maria, mama ya Yesu, alichukua mimba pasipo kuwa na tendo la ndoa.

## 5 Yesu hana zambi

Yesu alizaliwa na bikira na hakuteseka na hali ya zambi. Kwa maisha yake yote Yesu hakukuwa na zambi.

## 6 Umungu wa Yesu

Njia ya peke kwa mwandamu kurejeshwa kiroho kwa Mungu ilikuwa Mungu kujenga kilalo juu ya shimo iliyotenga mutu na yeye. Kwa hivi Mungu, akiwa na hali yake yote ya umungu, alifanyika mutu kabisa ndani ya Kristo ili kuzibia shimo. Ikiwa yeye si Mungu, mutu hataweza kupatanishwa kati yake na Mungu (1 Timoteo 2:5).

## 7 Umutu wa Kristo

Yesu alikuwa pya mutu kabisa. Yesu alichoka; alilala; alitoa jasho; alisikia njaa na kiu. Pasipo kuwa mutu kabisa, Yesu hangeweza kulipa bei ya zambi ya mwanadamu. Ilihitajika awe Mungu kwa kuwa na uwezo ya kutuokoa na ilihitajika awe mutu ili *achukue kweli fasi* yetu. Kristo alikuwa hivi mutu na Mungu.

## 8 Umuhimu ya neema ya Mungu

Kwa sababu ya kupungukiwa ya mutu, hatutaweza kujiokoa sisi wenyewe. Ni tu kwa neema ya Mungu peke yake ndio wokovu inawezekana. Mungu ni haki anapohukumu mutu kwa sababu ya zambi. Hata hivi, kwa neema yake, watu wale wasiostahili wataungana naye katika ushirika na yeye kwa kuepuka hukumu. Pasipo neema ya Mungu, hakuna mutu angefikia ushirika na Mungu.

## 9 Umuhimu ya imani

Imani ni kutumainia Mungu anaweza kutuokoa na atatukokoa. Hakuna mutu anayeweza kujipatia wokovu. Kazi nzuri hata ni kipimo gani haziwezi kulipa deni yetu kwa Mungu. Hata hivi, kwa kumutumainia Mungu na kukubali na aksante zawadi yake ya wokovu, tunaweza kuunganishwa na Mungu. Imani ni tendo toka kwetu, lakini si kazi. Imani ni kumutumainia Mungu kufanya ile hatungeweza kujifanyia (Waefeso 2:8–9; Tito 3:5–6).

## 10 Kifo cha Kristo kwa kulipa deni yetu

Hukumu ya zambi ni kifo—hapana tu kifo kimwili (kutengwa ya nafsi na mwili), lakini pya kifo kiroho (kutengwa na Mungu). Hukumu ile tulistahili kulipia Mungu ililipwa na Kristo kupitia kifo chake musalabani. Ilifaa malipo ya kukubaliwa iwe kamilifu, ya kutosha na pasipo kosa. Kristo, Mutu mukamilifu, alijitoa yeye mwenyewe kwa fasi yetu ili mutu yeyote anayemwamini asikufe (kimwili na kiroho), lakini awe na uzima wa milele (Yoane 3:16).

### 11 Ufufuko kimwili ya Kristo

Kifo ya mateso ya Yesu ililipa zambi zetu, lakini ile hatua haikutimilika hadi aliposhinda kifo kwa kufufuka kimwili ndani ya mwili ile ile (Yoane 2:19–21). Kwa sababu Kristo ni mushindi juu ya kifo na mufano wa kwanza ya mwili mpya ya utukufu, watu wote watafufuka na kuishi kwa milele mbinguni ao katika ziwa la moto.

### 12 Kupanda ya Kristo na mwili mbinguni

Kristo alikufa kwa ajili ya zambi zetu na alifufuka kimwili kwa wokovu wetu. Kisha siku makumi ine, alichukuliwa juu katika mwili kwenda mbinguni.

### 13 Maombi ya Kristo

Kupanda kwa Yesu mbinguni na mwili ilimupa fasi kutumika kama mupatanishi (ao kuhani mukubwa) mbele ya Mungu. Kwa uwepo wa Mungu, Kristo anatuombea wakati wote.

### 14 Kurudi ya Kristo mara ya pili

Ginsi Kristo alivyioacha dunia kimwili, vivyo hivyo atarudi. Kuja kwake mara ya pili ni tumaini ya dunia. Atakaporudi, waamini waliokufa watapokea miili yao ya ufufuko. Waamini walio hai hawatakufa, lakini watabadilika kwa miili ya kutokufa. Kurudi kwa Kristo kimwili duniani itakuwa wazi kwa watu wote na waamini watatawala pamoja naye katika ufalme wake na kuishi naye milele. Wasioamini watatengwa toka uzuri wa Mungu kwa milele.

**Kuamini ao kutokuamini?**

Si mafundisho yote yanayofaa kwa wokovu ni ya maana kwa mutu kuamini ili aokolewe. Kuna tofauti kati ya ile inapasa kuwa *kweli* ili tuokolewe na ile inapasa *kuaminiwa* ili tuokolewe. Kwa mufano, hakuna sehemu ndani ya Biblia inayosema ni lazima kuamini kuzaliwa ya Yesu na bikira kwa kuingia mbinguni; hata hivi kuzaliwa ya Yesu na bikira inatuhakikishia ya kwamba ni Mungu alivunja pingu ya zambi kupitia Mwana wake, Yesu. Kuna mafundisho zingine za muhimu yale mutu hataweza kujua ao kuamini waziwazi, na bado anaokolewa (kama kuzaliwa ya Yesu na bikira, kupanda kwa Yesu mbinguni na kurudi mara ya pili ya Yesu), lakini hii si kusema ya kwamba mutu anaweza kuzipinga. Kuna vile mambo mengie yale mutu anapasa kuamini waziwazi ili aokolewe. Mutu anapasa kuamini ya kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya zambi na alifufuka tena (Rom. 10:9; 1 Kor. 15:1–6). Mutu anapasa « kuamini Yesu Kristo » (Matendo 16:31). Neno « Bwana » (*kurios*) inapohusu Kristo katika Agano la Kale ikimaanisha « umungu, » hakuna mutu anayeweza kukataa umungu wa Yesu na aokolewe (Matendo 2:21, 36; 3:14–16; 5:30–35; 10:39; 1 Kor. 12:3).

Norman Geisler • *Essential Doctrine Made Easy* (Rose Publishing, 2007)



AC|FAR

Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Mafundisho ya kibiblia ya utatu takatifu

Mungu ni mumoja anayeishi katika ukamilifu ndani ya watu tatu. Kukuwa kwake ndio ni ile Mungu yuko, na uhusiano na ulimwengu aliyeumba. Watatu wale wanaitwa watu kwa sababu wanakuwa na uhusiano na kila mumoja kwa njia ya upeke.

Wakristo wanapozungumuza kuhusu kuamini Mungu mumoja ndani ya watu tatu (utatu takatifu), hawaamanishe:

Mungu 1 ndani ya Mungu 3, ao

Watu 3 ndani ya mutu 1, ao

Watu 3 ndani ya Mungu 3, ao

Mutu 1 ndani ya Mungu 3.

Lakini, wanamaanisha:

Mungu 1 ndani ya watu 3.

Kwa hivi,

Baba ni Mungu—Mutu wa kwanza wa utatu takatifu

Mwana ni Mungu—Mutu wa pili wa utatu takatifu

Roho Mutakatifu ni Mungu—Mutu wa tatu wa utatu takatifu.

## Kwa nini wakristo wanaamini utatu takatifu?

Biblia inafundisha wazi ya kwamba kuna Mungu mumoja tu, na watu watatu wote wanaitwa Mungu.

**Kuna Mungu mumoja tu:**

- « Sikia, Ee Israeli: Bwana Mungu wetu ni Bwana mumoja » (Kumbukumbu la Torati 6:4)
- « Mbele yangu hakuumbwaMungu, wala nyuma yangu hatakuwa mwingine » (Isaya 43:10; 44:6, 8; 45:5a).

**Baba ni Mungu:**

- « Neema kwenu, na salama toka Mungu Baba wetu, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo » (1 Wakorinto 1:3; 8:6; Waefeso 4:4–6).

**Mwana ni Mungu:**

- « Neno alikuwa Mungu (Yoane 1:1–5, 14). Yesu ametambulishwa kama « Neno ».
- « Mimi na Baba ni mumoja » (Yoane 10:30–33).
- Tomasi, mwanafunzi ya Yesu aliita Yesu « Bwana wangu na Mungu wangu » (Yoane 20:28). Yesu hakuambia Tomasi amekosa; Yesu alikubali majina haya. Watu wengine ndani ya Maandiko, zaidi Paulo na Barnaba (Matendo 14, walikataa kuabudiwa kama miungu.
- « Lakini juu ya Mwana anasema: Kiti chako cha ufalme, Mungu, ni cha milele na milele, na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki » (Waebrania 1:8).
- « Kwa hivi Mungu vilevile alimutukuza sana, na kumpa jina lililo juu ya kila jina; hata kwa jina la Yesu kila goti lipigwe,la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia, na kila ulimi ukiri ya kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba » (Wafilipi 2:9–11).

  Paulo, mwandishi ya Wafilipi, anasema kuhusu Yesu ile Isaya 45:23 inasema kuhusu Bwana, na Paulo anamaliza akisema ya kwamba Yesu ni Bwana—huyu ni, yule Bwana Mungu wa Agano la Kale.

# Mafundisho ya kibiblia ya utatu takatifu

Ona mashairi haya kuhusu umungu wa Yesu: Isaya 7:14; 9:6; Yoane 1:1; 8:58, 59; 10:30; Matendo 20:28; Waroma 9:5; 10:9–13; Wakolosayi 1:15, 16; 2:9; Tito 2:13; Waebrania 1:3, 8; 2 Petro 1:1; 1 Yoane 5:20.

## Roho Mutakatifu ni Mungu:

- « Lakini Petro alimwambia: Anania, kwa nini Shetani amejaza moyo wako kusema uwongo kwa Roho Mutakatifu … Hukusema uwongo na watu, lakini na Mungu » (Matendo 5:3–4). Hii shairi inaona Roho Mutakatifu ni Mungu.
- « Sasa Bwana ni Roho » (2 Wakorinto 3:17). « Bwana » hapa inahusu « Bwana » katika shairi la Agano la Kale (Kutoka 34:34) ile Paulo alitaja katika shairi ya mbele (2 Wakorinto 3:16).

## Zaidi ya mashairi 60 ya Biblia z inataja Watu Watatu pamoja

- Matayo 3:16–17 « Wakati Yesu alipobatizwa mara alitoka katika maji; na tazama, mbingu zikamfunguliwa, akaona Roho ya Mungu akishuka kama hua, akikuja juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. »
- Matayo 28:19 « Kwenendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu; »
- 2 Wakorinto 13:14 « Neema ya Bwana Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae pamoja nanyi nyote. »
- Waefeso 4:4–6 « Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na vilevile mulivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu; Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba ya wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote. »
- Tito 3:4–6 « Lakini wema wa Mungu Mwokozi wetu, na mapendo yake kwa watu yalipoonekana, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyofanya lakini kwa rehema yake, alituokoa, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa mpya na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; ambaye alimwaga juu yetu, kuzidi sana, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu… »

Ona vile Yoane 3:34–35; 14:26; 15:26; 16:13–15; Waroma 14:17–18; 15:13–17, 30; 1 Wakorinto 6:11, 17–19; 12:4–6; 2 Wakorinto 3:4–6; Wagalatia 2:21–3:2; 4:6; Waefeso 2:18; 3:11; 5:18–20; Wakolosayi 1:6–8; 1 Watesalonika 1:1–5; 4:2, 8; 5:18–19; 2 Watesalonika 3:5; Waebrania 9:14; 1 Petro 1:2; 1 Yoane 4:13–14 na Yuda 20–21.

*The Trinity* (Rose Publishing, 1999)



AC/FAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Vikundi sita ya mafundisho ya uwongo

Hali ya mafundisho ya vikundi ya zehebu (*secte*)

**1 Ufunuo**—mafundisho zinazoharibu, kukataa ao kuongeza kwa Andiko kwa njia inayoongoza watu katika uharibifu; mambo ya uwongo kuhusu kuwa na mamlaka ya mutume ao nabi.
*Mifano:*




- **Mormonisme** (Joseph Smith kama nabi; *Kitabu ya Mormon* na « maandiko » mengine ya Mormon).
- **Mashahidi wa Yehovah** (Mungu anazungumuza tu kupitia Jamii ya Munara wa Mlinzi; « jamii ya mupakaliwa » peke yake inaweza kueleza Biblia).
- **Adventiste ya siku ya saba** (Ellen G. White kama nabi ya peke ya Mungu kwa wakati wa mwisho).

**2 Mungu**—mafundisho yanayoendelesha miungu ya uwongo ao uharibifu ya hatari ya ukweli ya Mungu. *Mifano:*

- **Mormonisme** (kuna miungu mingi; Mungu Baba alikuwa mutu aliyepungukiwa kwa dunia ingine; tunawezakuwa miungu ginsi alikuwa).
- **Mashahidi wa Yehovah** (Utatu takatifu ni uwongo, kwa sababu Baba peke yake ni Mungu).
- **Pentekote ya upeke** (Utatu Takatifu ni uwongo, kwa sababu Yesu ni Baba, Mwana *na* Roho Mutakatifu).

**3 Kristo**—kukataa upeke wake kama Bwana, ukweli ya umutu wake, hali yake ya kweli. *Mifano:*

- **Mashahidi wa Yehovah** (kwanza Yesu Kristo alikuwa malaika mukubwa Mikaeli, kasha mutu kamilifu - hapana Mungu katika nyama)
- **Mormonisme** (Yesu hakuzaliwa na bikira, kwa sababu Mungu Baba alikuwa na tendo ya ndoa na Maria kwa kuzaa mwili ya Yesu)

**4 Wokovu**—kufundisha sheria ao ruhusa ya kutenda zambi; kukataa habari njema ya kifo cha Kristo na ufufuko wake; etc.
*Mifano:*

- **Mormonisme** (mashurti yanakuwa kwa sisi kutimiza kustahili ya binafsi pamoja na kuamini Joseph Smith kama nabi ya Mungu)
- **Mashahidi wa Yehovah** (katika mashurti ni kutumikia kutmikia chama moja ya kweli ya Jehivah, Jamii ya Munara ya Zamu).

**5 Kanisa**—kuchagua kuongoza watu mbai na ushirika ya wakristo wa kweli; kutangaza kukataa kanisa.
*Mifano:*

- **Mormonisme** (kanisa zingine zote za « Kikristo » ni za uwongo na mafundisho yao ni « machukizo » kwa Mungu)
- **Branhamisme** (wakristo wote wa kweli wanapasha kuacha kanisa zao na kufuata William Branham, nabi ya kweli ya Mungu ya mwisho ya wakati).



**6 Mambo ya kuja**—unabi ya uwongo wakisema inatoka kwa Mungu; wakisema ya kwamba Kristo amerudi tayari, etc.
*Mifano:*

- **Mashahidi wa Yehovah** (falsely predicting Jesus' return [1874, 1914] and Armageddon [1941, 1975])

Robert M. Bowman, Jr.

# Maandiko kuhusu uchawi

Katika Agano la Kale na Agano Jipya, Mungu anaagiza watu wake kuepuka uchawi ya aina yote—kwa njia ya ukali sana. Mara kwa mara Biblia inafananisha uchawi na kuabudu sanamu, udanganyifu, woga, jambo isiyo na maana, uchafu na uasi. Mungu anaona mambo haya kama ubaya, ya kishetani na yanastahili mapigo na hukumu.

SHIKA: Katika Biblia maneno sawa katika Kiebrania na Kigriki yanaweza kutafsiriwa katika Kiswahili kama uchawi na ulozi.

## Biblia haikubali uchawi

Mwanzo 41:8, 24
Kutoka 7:11, 22; 8:7, 18–19
Walawi 19:26
Kumbuku la Torati 18:10
2 Wafalme 17:17; 21:16
2 Mambo ya Siku 33:6
Isaya 47:9, 12
Yeremia 27:9
Matendo 8:9–11; 18—21; 13:6—12; 19:19
Ufunuo 9:20, 21; 18:23; 21:8; 22:15

## Biblia inakataza kutumia vitu vya uchawi

Isaya 3:18–20
Ezekieli 13:18–20

## Biblia inahukumu ulozi

Kutoka 22:18
Walawi 19:26
Kumbukumbu la Torati 18:10, 14
2 Wafalme 17:17; 21:6
2 Mambo ya Siku 33:6
Isaya 47:9
Yeremia 27:9–10
Mika 5:12
Nahumu 3:4
Matendo 8:9–11; 19:19
Wagalatia 5:19–21
Ufunuo 9:21; 18:23; 21:8; 22:15

## Biblia inahukumu uroho (*spiritisme*), kuenda kwa wafumu na kwa wafu

Walawi 19:31; 20:6
Kumbukumbu la Torati 18:10–11
1 Samueli 28:3, 9
2 Wafalme 21:6; 23:24
1 Mambo ya Siku 10:13
2 Mambo ya Siku 33:6
Isaya 8:19; 19:23
Yeremia 27:9

## Biblia inahukumu kutumia ubashiri

Kumbukumbu la Torati 18:9–11
Isaya 47:9, 12
Mika 5:12

## Biblia inahukumu maaguzi

Walawi 19:26
Kumbukumbu la Torati 18:10, 14
1 Samueli 15:23
2 Wafalme 17:17; 21:6
2 Mambo ya Siku 33:6
Isaya 2:6
Yeremia 27:9–10
Matendo 16:16–20



AC|FAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Maandiko kuhusu uchawi

**Biblia inahukumu uchawi**
(hii haihusu dini Fulani yap eke, lakini kwa matendo ya uchawi kwa jumla)

Kumbukumbu la Torati 18:10, 14
1 Samueli 15:23
2 Wafalme 21:6
2 Mambo ya Siku 33:6
Mika 5:12
Nahumu 3:3–4
Wagalatia 5:19–21

**Biblia inahukumu kuabudu mwezi, nyota na jua (astrologia)**
Kwa sababu ni aina ya uchawi, astrologia inakatazwa katika maandiko kama Walawi 19:26 (« …wala musifanye kuloga wala kutumia uaguzi »). Tunapata pya mwangaza toka mashairi kama

- Isaya 47:13–15 (« Umechoka kwa wingi wa mashauri yako. Sasa wale wenye ya kujua elimu ya nyota, nao wanaotazama nyota, wanaotabiri kila kundama kwa mwezi, wasimame na kukuokoa wewe toka maneno haya yatakayokupata. Tazama, watakuwa kama mashina makavu ya majani, moto utawateketeza; watajiokoa na nguvu za ulimi, wala mo wa moto; hautakuwa kaa la kuota moto wa kukaa karibu nao. Ndivyo yatakavyokuwa mambo haya uliyojitaabisha nayo, waliofanya biashara nawe tangu ujana wako watatangatanga kila mutu upande wake; hatakuwa mutu wa kukuokoa » wamezarauliwa na kuhukumiwa)
- Yeremia 8:1, 10:2 (wale wanaofuata, wanaoabudu, wanaotafuta toka jua, mwezi na nyota wamehukumiwa)
- Danieli 2, 4, 5 (kisha wale wanaoabudu nyota, mwezi na jua na wachawi wengine wanasema ya kwamba kutafsiri ndoto za Nebukadeneza na Belsasari ilikuwa jambo ngumu, Danieli anaweza kupitia usaidizi ya Mungu).

*Christianity, Cults, and the Occult*
(Rose Publishing, 2006)



## Kwa nini inafaa kujiuliza kuhusu kuabudu mwezi, nyota na jua?

Katika kitabu chake *Wisdom from India: Astrology* (Hekima toka India: Kuabudu mwezi, nyota na jua), Vishal Mangalwadi, mukristo mwenye kupigania imani, anaona mambo matatu kwa sababu gani astrologia inachukua nafasi kwa wakati ya mateso:

- Inaleta maelezo kuhusu mateso yetu
- Inaondosha mafikili ya kujilaumu na ya mapashwa
- Inaleta uongozi wakati watu wanajiona pasipo msaada.

### Nini inafanyiza astrologia « kutumika »

Si tu ya kwamba astrologia inakataliwa ndani ya Biblia—ni ya kishetani. Charles Strohmer, muastrologia wa zamani, ameandika katika kitabu chake *What Your Horoscope Doesn't Tell You (Nini horoscope yako haikuambii):* « Tukiona kwa uaminifu astrologia, tunaona ya kwamba wafuasi ya astrologia—pasipo kujua—wanagonga mulango kupitia wapi mazungumuzo yanafanyika kwa kujua lakini na vyumbe ya kudanganya. » Anaeleza zaidi ya kwamba chombo ile watu wa astrologia wanatumia inaweka uhusiano na vyumbe vingine na ya kwamba « pasipo na uhusiano na vyumbe vya kiroho, hakutakuwa na siri ya astrologia itakayoonekana. »

# Mambo 10 kwa kuhubiri wanamemba ya vikundi za *sectes*

1 **Kujua mafundisho ya musingi ya Biblia.** Hakuna mutu anayeweza kujua kila mafundisho ya uwongo ya kila zehebu, lakini wakristo wale wanaojifunza Biblia vizuri, wanaweza kujijenga kutambua mafundisho ya secte. *Jua nini unaamini na kwa nini.*

2 **Usizani ya kwamba wanamemba wote ya secte wanaamini jambo sawa.** Wafuasi ya kikundi moja wanaweza kuwa na tofauti katika kujua kwao. *Uwaulize* kuhusu imani yao; usiwashitaki.

3 **Wafuasi ya secte wamefundishwa kujibu wakati wanawapinga.** Kwa mufano, Mashahidi wa Yehovah na missionnaires za Mormon wanaonekana kuwa na jibu kwa kila ulizo. Lakini mara nyingi ile wanajua *kwa kweli* ni tu mafundisho yao, mambo machache ya Biblia na ginsi ya kuzungumuza ile walijifunza inafanyiza waonekane kujua zaidi kuliko ile wanajua kwa kweli.

4 **Chunguza Maandiko.** Mara mingi watu ya secte wanataja mashairi ya Biblia inje ya ile imeandikwa ndani ya Biblia (contexte).

5 **Maana.** Mazehebu (sectes) zinaleta maana mpya kwa maneno ya kawaida kama « Mungu » na « wokovu ». Unaweza kutoa ile inayokutenga na wale wanamemba ukieleza vizuri sana maana ya maneno na mafikili muhimu ndani ya dini ya kikristo.

6 **Uliza maulizo ya maana.** Hautaweza kusukuma mafundisho mazuri kwa mutu anayekuwa katika mutego ya kikundi ya secte. Ila, uliza maulizo yale yanayoweza kumusaidia kufikili.

7 **Uwe na upendo.** Si tu *ile* unasema, ni *namna gani* unaisema ! Uwe na namna ya kukaribisha na heshima kila mara, hata kama wao hawako. (Vikundi vingine wanatarajia vita na kukosa heshima).

8 **Onyesha umungu ya Yesu.** Watu wa zehebu kila mara hawatambui vizuri hali ya Yesu, wakikana ao kuharibu umutu wake na kazi yake. Jua Maandiko yale yanaonyesha ya kwamba Yesu ni Mungu.

9 **Weka mkazo juu ya Habari Njema.** Watu wa zehebu wanahitaji kusikia ukweli kuhusu neema ya Mungu zaidi kuliko jambo lingine lolote.

10 **Toa ushuhuda yako.** Mungu anaweza kutumia historia ya ile Yesu Kristo alifanya katika maisha yako kwa kubadilisha nia na roho.

Ron Rhodes • *10 Keys to Witnessing to Cults* (Rose Publishing, 2008)



AC|FAR

Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Namna gani na kwa sababu gani vikundi ya secets zinavuta watu (hata wakristo)

**Uwezo mbili**

1. *Njia mbalimbali* secte inatumia kwa kutafuta watu, kuwabadilisha, kubadilisha mafikili yao na kubaki na wanamemba yao.

2. Hali yakutosimama imara ya yule wanaweza kumuingiza katika secte

   a. Hadizi isiyo kweli: Watu wengi wanaoingia ndani ya secte ni wale hawajiwezi ao « wale wamepoteza ».

   b. Ukweli: Mara nyingi sectes zinavuta watu wa akili na wale wanaoneka vizuri. Hata hivi, watu wale wanaokuwa katika hasara ao wanaokuwa na shida ya mafikili (kama kuachana katika ndoa ao kifo katika jamaa) wanaweza kudanganywa haraka na wamisionari za sectes ao wanamemba (kikundi inaweza kutumia kwa akili sana lugha ya mapendo ya wale watu ginsi inavyosemwa na Gary Chapman).

   c. Uchunguzi ya chini sana: « Kuna njia inayoonekana kuwa sawa kwa macho ya mtu; lakini mwisho yake ni njia ya mauti. » (Mezali 14:12)

   d. Mahitaji yasiyotimilika: « Lakini kwa nafsi yenye njaa kila kitu kichungu ni kitamu. » (Mezali 27:7b)

**Sababu mane ya musingi kwa nini watu wanajiunga na sectes**

1. Kusoma
   Kupata majibu kwa maswali ya musingi ya Biblia na maisha kwa njia ya akili; rahisi kwa mafundisho mingi ya uwongo kutokana na kusoma—mufano, Mashahidi wa Yehovah.

2. Kuguza moyo
   Hitaji ya mapendo, kwa kusimama katika hali ya kuhurumiwa, « jamaa ».

3. Kijamii
   Hitaji ya kuwa na kazi na kujulikana katika kikundi ile inayoongoza jambo fulani ya maaana sana.

4. Kiroho
   Kutafuta kuwa karibu sana na Mungu, kwa mambo ya ajabu na miujiza, kwa kanisa « ya kweli ».



**Hatua tatu**

1. Kudanganywa (mbele ya kuingia)
   Kikundi inaleta ahadi za uwongo, inaficha hali yake ya kweli, inaondoa habari mbaya inayohusu kikundi.

2. Kutegemea (unapokuwa mpya ndani ya kikundi)
   Kikundi inakufanya kupoteza tumaini yote na inakutenga na jamaa, rafiki zako na watu wengine wangeweza sana kukushurulikia kama mufuasi ya ile kikundi.

3. Kusumbuka (wakati ikiendelea)
   Kikundi inakufanyiza kuogopa sana kwa kupata mambo mabaya ya kiroho na kijamii ikiwa utachagua kuacha. Katika sectes nyingi, *hakuna* njia ya heshima ya kutoka naye na unaweza kupoteza kila kitu (pamoja na jamaa, rafiki zako, kazi yako na mali yako) ikiwa utaenda mbali na kutaka ya kikundi na kuondoka.

Michael Langone • Harold Busséll

# Hatari ya kuingia ndani ya secte

Kuna dini nyingi za uwongo kwa Congo na katika dunia kwa jina ya kutangaza ukweli ya Mungu, lakini zinazoweza kuwa mwanzo ya umasikini ya maisha muzima, kuvunja jamaa, ugonjwa ya kichwa, kuacha masomo, ugonjwa kwa mwili ao mambo yasiyo ya kawaida katika mwenendo.

Tukienda leo kwa masomo na kuuliza mwanafunzi mukristo kuacha masomo na kuketi nyumbani akiongoja ufunuo wa Mungu, ni ngumu hata mwanafunzi moja kukubali. Nikifika kwake kama mwanamuke mwenye ameolewa na kukuambia kuacha mume wako kwa sababu yeye si mapenzi ya Mungu kwa maisha yako, hakose unaweza kuita police kuja kunifunga ao kuita muchungaji wako kwa simu na kumwambia ya kwamba nilikuwa nikikulazimisha kuvunja ahadi uliyofanya mbele ya Mungu. Kama nilikuuliza kufunga biashara yako na kunipatia pesa yote, ungeweza hakose kunipiga. Na kama ningekuuliza kukunywa mukojoo yangu, ungeenda kwa mahakama.

Mwaka moja ao miaka mbili tangu sasa, watu wengi—wanaosoma na wasiosoma, watajiri na masikini, waongozi na wanaoongozwa—wataanguka katika mambo haya kwa njia mbalimbali. Ninajua mwanafunzi moja ya chuo kikuu ya Nairobi aliyeacha masomo yake ya ujengaji mbele ya mitihani akiamini ya kama Mungu alimuita kurudi na kukaa nyumbani akingojea mapenzi yake. Ninajua mutu moja alyetumika na shirika ya barua (posta) aliyeacha kazi akitaja ile mafikili ya kwamba dunia imekaribia mwisho na hakukua na faida kuendelea kutumika. Ninajua wasichana wengi waliokuwa wakienda kwa mukutano ya « nabi » moja aliyewauliza daima waache waume wao na kurudisha pete zao ya arusi kwa sababu waume wale hawakuwa mapenzi ya Mungu kwa maisha yao. Waongozi wachache ya Mashahidi wa Yehovah walijukana kuuliza wanawake ao waume kuacha ndoa zao ikiwa mumoja anakataa kuwa Mushahidi. Mbele ya moto




ya Kanungu wapi karibu watu elfu moja walikufa, mwogozi ya « Restoration of the Ten Commandments » (Kurejeshwa ya Amri Kumi) aliuliza wanamemba kuuzisha vitu vyao, kufunga biashara na



AC/FAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

kumupatia mapato kwa sababu dunia ilikuwamalizika na utawalo wa miaka elfu moja.

Kwa hivi, nini ingefanya mutu fulani kutokuamini ao kukataa kutimia ya mambo haya, lakini kisha mwaka moja ao miaka mbili kutia moyo watu wengine kujiunga na dini yao ya kupoteza? Ni jambo ndogo sana: « Mungu anasema. » Mara hapo tu jina ya Mungu imetajwa, macho yetu na masikio yetu ya ufahamu zinafungwa na hamu yetu ya kujua inaamuka. Ni rahisi sana wakati yale masemo Mungu anasema zimejaa na ahadi za vitu ao cheo. Mara ingine ni kuhusu ahadi ya hali ya kiroho wapi mutu anaahidiwa kupanda cheo kiroho, akijulikana sana kuliko wengine waliokuwa naye katika shirika moja. Kuona ya kwamba Biblia inatajwa, wengi wanaacha ngozi yao ya kuchunguza. Ndio maana, mwanafunzi ao mwalimu anawezakuwa na akili sana kwa shule, lakini kutumia vibaya mambo ya kiroho inaweza kupunguza uweo yao ya kuchunguza. Hapa ndio kuna lazima ya kujifunza Biblia kila mara ili wadanganyifu wasitumie mashairi ya Biblia kwa njia mbaya na kuvutia watu wengi.



## Hatari zingine ya kuingia katika mambo ya *secte*:

**1. Sectes zinaweza kukuongoza kaburini.** Mara nyingi kupitia mahubiri juu ya maneno ya mwisho yanayoweka mkazo juu ya kurudi upesi ya Kristo, lakini sana kuhusu kwamba dunia itamalizika, vikundi kama hivi vilisukuma watu wengi kunywa sumu, sawa ile iliyotendeka kwa mwaka wa 1978 pale Jonestown, Guyana wapi Jim Jones aliongoza watu 913 kunywa sumu. Moto ya Kanungu iliacha karibu wafuasi 1.000 ya Joseph Kibwetere kufariki. Inawezekana kama « Nyumba ya Mungu » haikukatazwa kwa Kenya, watu wengi wangeangamizwa. Sectes zingine zinaweza kukataza watu chakula kwa muda ya siku nyingi ao kuwatia moyo kufunga chakula pasipo mwisho. Hii inamalizika na kukulishwa vibaya ao kupeleka watu kwa kifo. Katika dunia inayojaa na watu wale wanakuwa na bomu na tayari kujiua na kuua wengine wakiamini wanatenda uzuri kwa Mungu—waliosoma sawa na wasiosoma—hatutaweza kuzungumuza zaidi kuhusu jambo hilo.

**2. Sectes zinaweza kuvunja nyumba yako kesho.** Mapema kwa miaka za 1990 nilijua mutu moja kwa Thika (Kenya) yule mwanamuke yake alikuwa akienda kwa secte fulani. Alifundisha sana kufikia hatua aliona jamaa yake kama adui ya mwito ya Mungu kwa yeye.

# Hatari ya kuingia ndani ya secte

Aliacha nyumba yake wakati musichana wake alikuwa tu na miezi chache. Alipoona nuru, huyu musichana alikuwa karibu miaka kumi. Rafiki na jamaa, police na watu wengine waliomutakia mema walijaribu sana kumurudisha nyumbani, pasipo kuweza. Nilikuwa nikizungumuza kwa Teso miaka mingi zilizopita wapi niliaambiwa kulikuwa na kikundi iliyokuwa ikisambaza nyumba za wengi kwa jina la Mungu. Mara zingine wanawake walitiwa moyo kuacha waume wao na kuwa wake ya mwongozi ya secte.



**3. Sectes zinaweza kukufanyiza masikini kwa haraka.** Ile inayoitwa Habari Njema ya Kuendelea ni katika nyumba za wakristo wengi. Wanaume na wanawake wa tamaa wanaojifanya kama watumishi wa Kristo wanasafisha pesa za watu na kuwafanya watumwa kwa jina ya kumutolea Mungu.

Maandiko kama Malaki 2:16 na Luka 6:38–39 zinatumiwa kwa njia mbaya kwa kuiba maelfu za watu ile mali wanapata katika shida sana. « Toa hadi inauma » na « usimutolee Mungu ile haina maana kwako, » « jaribu Mungu na ona kama hatakubariki » na zaidi sana, « bariki mutumishi wa Mungu » ni maneno yanayotumiwa kwa kudanganya mutu mwaminifu. Shida ni ya kwamba wakati wengi wanatoa hata pesa yao ya transport, mishara na mali, ila tu wale wanapokea ndio wanaendelea, hapana wale wanaotoa. Njia moja ya kupata waamini ni kutumia vibaya andiko ndani ya Marko 10:29-31 wanapoambiwa ya kwamba wakitoa watapata zaidi ya mara makumi sita na zaidi ya mara mia. Tena, waamini wengi wanchomwa sana na mafikili ya kupokea kwa kiwango wanadanganywa kwa urahisi kupeleka mali yao. Inatupasa kufanya angalisho sana kuhusu ahadi zinazosema kupokea kwa haraka ile ulitoa. Kumbuka masemo: Kama mapatano fulani ni muzuri sana, fikilia mara mbili. Fanya angalisho kwa kulipa pesa kwa ajili ya maombi. Fanya angalisho kuhusu « kupanda mbegu ya pesa » na ujinga ya sasa kununua mafuta ya upako. Hizi ni michezo za uchumi, hapana kuweka kwa njia ya kiroho.



Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

AC/FAR

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

**4. Sectes zinaweza ongoza kwa magonjwa kimwili na kimafikili.** Watu wengi wanaosihi mahali ya sectes wanalishwa na vyakula visivyiotosha kwa afya. Watu wengine walioishi kwa ile hali walianza kupata ndoto za kuogopesha na akili kuharibika. Wengine kati yao hawakufaa tena kwa jamii. Katika jimbo la Nyanza kwa Kenya, kwa mufano, wengine walitembea na waongozi za sectes na walipata ukimwi. Kwa Uganda na mara mengine kwa Kenya, ilibidi waongozi ya inchi kuenda kuokoa watu walioshikwa na zile dini. Mwenendo ya kuogopesha iliingiza wanamemba katika zile dini kuwika kama imbwa ao kunguruma kama simba kama alama ya kuangazwa kiroho ao ya kuabudu. Hali ya kawaida ya wanamemba ni kuingia katika kuchanganyikiwa ya akili inayoongoza mara nyingi kwa kifo.

## Mashauri kwa kuzuia hatari za sectes

Kwanza, **wazazi wangeanza kufundisha watoto wao Neno la Mungu mapema sana.** Njia nzuri



sana ni kujifunza Biblia katika jamaa. Watoto wanapojua viuri Biblia, ni nguvu wadanganywe. Wazazi wanapofundisha Neno la Mungu, wataangaziwa vilevile na watajua mengi.



Ya pili, **kila mutu anapasa kuwa na Biblia na kuisoma.** Wale wazazi wao ao wanamemba ya jamaa wamesoma wanaweza kufanya yote ile wanaweza kuwa na uhusiano na Societe Biblique kwa kupata Biblia kwa kusikia ao katika picha.

Ya tatu, **tunapasa kuwa na mafikili ya kuchunguza na kujua kuuliza maswali kuhusu kila jambo mbele ya kuamini.** Moja ya njia ya kuvuta watu ndani ya sectes ni kutaka kujua

Ya mwisho, **tuachae kutaka kuendelea haraka na kupata mali pasipo kuitumikia.** Tunapasa kukumbuka ya kwamba Mungu si kama machine wapi tunatoa pesa. Tunapasa jifunza kumuabudu. Zaidi ya yote, lazima tukimbie mbali na vikundi vinavyoonekana kuvutia kwa njia ya kufurahisha na kupendeza. ***Tukipenda Neno, tutatambua uwongo haraka.***

Reuben Kigame (Word of Truth Ministries/Kenya)

# Kuchunguza mafundisho ya musingi

Katika dini zingine za kikristo leo, kuchunguza mafundisho ya musingi ni jambo lisolitiwa moyo kabisa. Kuna watu wengine wale hawafurahie wale wanaotafuta kuchunguza mafundisho ya musingi ile wengine wanaamini. Sababu ya kufanya hivi, mara nyingi, ni rahisi: mafundisho yao hayawezi kusimama mbele ya mafundisho ya Biblia.

Tutarajie ya kwamba vikundi ya dini wanaokubali mafundisho ya uwongo na wanaojidai kuwa wakristo wa kweli, watakata watu moyo kwa kujitoa kuchunguza kati ya mafundisho ya kweli na ya uwongo. Ya kusumbua sana ni ya kwamba watu wengi kati ya wale wanasimamia Biblia wanakataza pya watu kuchunguza. Tunatoa hapa mambo yale wanafanya.

## « Usigawe mwili wa Kristo »

Pahali popote mafundisho ya mukristo fulani ya kujulikana ao ya mwongozi yanatiwa shaka, uwe na uhakika ya kwamba utakuta mutu atakayekuambia jambo kama hilo linagawa Mwili wa Kristo. Mwenye anachunguza anashitakiwa « kupanda mbengu ya matengano kati ya ndugu » (tangamano inayosimama juu ya Mezali 6:19), kuwa mwenye kugawa watu na kuleta matengano. Mara ingine, wana haki.

Ukweli ni ya kwamba mara mengine wale wanaochunguza mafundisho ya wengine wanakuwa tu na nia ya kupinga. Mara mengine watu wanaleta shida nyingi wakipandisha sana tofauti kati ya mafundisho. Magawanyiko ni zambi; ni lazima sisi wale tutafuta kuchunguza mafundisho tujichunge sana na magawanyiko.

Tukisema haya, magawanyiko yote si mbaya. Wakristo wanahitaji kujitenga na wasio wakristo. Hii ni jambo la kwanza. Ikiwa kundi ya watu fulani inasimama kanisani na inaanza kufundisha mafundisho tofauti na imani ya kikristo kwa kiwango kwamba ni ngumu kuona wale wanayoifuata kuwa wakristo wa kweli, kanisa ina *madaraka* (hapana tu *haki*) kujitenga na kikundi kama ile.

Kwa kweli, ijapokuwa wale wanaoamini mafundisho ya uwongo wanaweza kuwa wakristo, makosa ikiwa mbaya sana, kanisa inapasa kusimamia mafundisho ya kweli inayotoa makosa na wale wanaoifundisha.





Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

AC/FAR

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Kuchunguza mafundisho ya musingi

Katika Waroma 16:17 Paulo anaandika, « Ninawasihi ninyi, ndugu, aangalieni wale wanaofanya matego na mambo ya makwazo, *mbalimbali na mafundisho muliyofundishwa*; mugeuke kotoka kwao. » Kulingana na Paulo, ni nani mwenye kuleta magawanyiko? Ni wale wanaofundisha uwongo ao wale wanaotaja wenye kufundisha uwongo? Ni wazi, ni wale wanaofundisha uwongo. Wale « wanapiga firimbi » juu ya walimu ya uwongo kanisani *si* wale wanaoleta magawanyiko.

Tuione kwa njia ingine. Fikilia ya kwamba katika kanisa moja kuna vikundi mbili ya watu. Kundi ya kwanza inakubali mafundisho kanisa ilitoa kwa muda ya miaka mingi tangu ianzwe. Kundi ya pili inafuata mafundisho iliyoingiwa na mwalimu mupya ya uwongo. Mafundisho haya mawili ni tofauti kabisa—kwa kiwango ile tunaweza kusema zinakuwa na mafikili mbili tofauti ya kuwa mukristo. Kwa hali kama hii, tuna nini? Tayari tunakuwa na magawanyiko kanisani. Si ya kuepuka. Vikundi mbili haviwezi tena kutumika pamoja. Ikiwa mafundisho ya imani yao ni tofauti sana, watakuwa na ufahamu isiyoambatana kuhusu ni nini inatendeka katika maombi, hata hawataweza kuomba pamoja.

Sasa, kwa hali kama hii, hakuna shida kutaja na kukubali nini inaendeka. Kukubali ya kwamba kuna magawanyiko si kuingiza magawanyiko. Pya hakuna shida kukubali mafundisho ya kundi moja ni kweli na ingine ni uwongo. Kwa mwisho, wote wanaweza kuwa na haki yao.

Tuwe na uhakika ya kwamba hatugawanyike kwa maneno yasiyokuwa na maana. Kwa upande mwingine, umoja hata kwa bei gani haitawezekana. « Umoja ya imani » inapaswa kuchungwa katika kukubaliana na kujua kwa kweli mafundisho ya Biblia (Wefeso 4:15–16). Mara nyingi walimu wale wanaohuzunikia magawanyiko ya mwili ya Kristo ni wale tayari wameigawanya kwa njia ya kufundisha uwongo.

## « Usiguze mupakaliwa wa Mungu »

Wakristo wanapoeleza kushurulika kwao kuhusu mafundisho ya musingi kufundishwa na wahubiri wakristo wanaofaa, mara mingi unasikia, « Usiguze mupakaliwa wa Mungu! ». Mara mbili katika Biblia tunasoma Mungu akisema, « Musiguse wapakaliwa wangu, na musizuru manabii wangu » (1 Mambo ya Siku 16:22; Zab 105:15). Hii inapotumiwa na walimu wengine leo, maana yake ni ya kwamba hakuna mutu yeyote ila Mungu tu ana haki ya kuhukumu ao ya kusema kwa wazi mafundisho ya walimu wengine wanaojulikana kama « wapakaliwa » wa Mungu.

Tutafahamu hii namna gani? Ndio, pahali ya kuanza ni katika maandiko. Ginsi inavyoandikwa, « wapakaliwa »

ni wale wababa ya zamani—Abrahamu, Isaka na Yakobo (Mambo 16:15–21; Zab 105:6–14). Si wazi kwa sababu gani wanaitwa « wapakaliwa wa Mungu ». Inaonekana nono « wapakaliwa » ni sawa na « nabi » kwa mustari wa pili. Ijapokuwa matumizi hii si sana ndani ya Biblia, inaweza kupatikana (1 Wafalme 19:16b; Isa 61:1). Inaambatana pya na wakati na pahali (contexte) imeeandikwa, kwa sababu mukazo ni juu ya kazi wababa wa zamani walifanya kama wale waliotumiwa kupitisha Neno la Mungu, agano kwa kufanya wana wa Israeli.

Kwa upande ingine, ni wazi ya kwamba wababa wa zamani walikuwa *zaidi* ya nabi. Walikuwa watu wale waliahidiwa ya kwamba uzao yao utakuwa na wafalme watakaoongoza muji wa Kanana (Zab 105:11; Mwa 17:6, 16; 35:11). Hii ni wazi, kwa sababu wakati Agano la Kale inazungumuza kuhusu wafalme, inawataja (mufano, 1 Sam 2:10, 35; 2 Sam 1:14, 16; Zab 2:2; 89:38, 51; Dan 9:25, 26; ona 1 Sam 16:12, 15; 1 Mamb 11:3, 14:8, 29:22; Isa 45:1).

Kwa njia yoyote, « wapakaliwa » wale Mungu alisema « wasiguzwe » haikukuwa tu walimu, wahubiri, waenjilisti ao waongozi wa dini. Walikuwa watu wa peke katika historia ya Israeli wakiwa na uwezo ya unabi na mamlaka ya kifalme na maana.

Sasa, kuna walimu wengine wanajidai pya kuwa nabi—watu wa maana wale Mungu anatumia kwa kuzungumuza leo. Lakini, watu wengine wanasema « usiguze wapakaliwa wangu » na kwa urahisi sana wanaitumia kwa mutu *yeyote* wanafikili ana zawadi ya Roho kwa kufundisha ao kwa utumishi. Jambo kama hii haiambatane na maana ya andiko.

Neno lingine ile inahitajika hapa ni ya kwamba Mungu alikataza wafalme wapagano kuua ao kutenda ubaya kwa « wapakaliwa » wa Mungu. Mungu hakukataza watu kuchunguza wapakaliwa wake. Kwa mufano, katika Mwanzo 20:7 Mungu alitoa angalisho kwa Abimeleki, mufalme wa Gerari, kurudisha Sara kwa Abrahamu, « kwa nabi yake ». Lakini hii haikukataza Abimeleki kuuliza Abrahamu kwa nini alidanganya (shairi 9–10). Ni jambo moja kutenda ubaya kwa wapakaliwa wa Mungu; ni jambo lingine kuwachunguza wanapokosa. Hata manabi ya kweli wasiposema ukweli, wanawezakosa (mufano, 2 Sam 7:3; ona shairi 4—17).

Ni kweli hatuwezi kukataa manabi wa Mungu; mapaswa yetu ni kuhakikisha wanani ni manabi ya kweli wa Mungu. Si mutu yeyote anayesema leo yeye ni nabi wa Mungu anaweza kuwa kweli nabi, kwa sababu mara mingi wanapingana.



AC|FAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Kuchunguza mafundisho ya musingi

Ikiwa mutu anasema yeye ni nabi ya Mungu na anafundisha mafundisho mabaya ao ananaba uwongo, tuna haki yote ya kumukataa—kwa kweli, tunapasa kuwakataa (Tor 13:1–5; 18:20–22).

Katika Agano Jipya, Mupakaliwa ni Yesu Kristo, aliye nabi, kuhani na mufalme wa *kweli*. Wote wale wameungana na Kristo kupitia Roho yake ni, kwa njia ingine, « wapakaliwa » (2 Kor 1:21). Kwa hivi, hatuhitaji walimu « wapakaliwa » wanaokuwa na siri ya ufunuo ya kujua wakisema wanakuwa na mamlaka ya upeke na kutuambia kuwatumainia (1 Yoane 2:20, 27).

Jambo ya musingi ni: Agano Jipya inatuambia wazi kujaribu walimu wa uwongo kanisani (Rom 16:17; 1 Tim 1:3; Tito 1:11, 3:10–11). Kwa hivi, hakuna mutu anayekuwa na haki kujificha akisema yeye ni « mupakaliwa wa Mungu ». Ikiwa mutu anafundisha uwongo, hii inatosha kuonyesha ya kwamba yeye si mupakaliwa wa Mungu.

## « Chunguza tunda! »”

Mutu akiwa mwalimu ya kweli ao ya uwongo, ni mafundisho yake ndio itaonyesha. Watu wengine hawakubali hii. Wakristo wengine leo wanasema ya kwamba walimu na watumishi wanapasa kuhesabiwa kulingana na « tunda » ya utumishi yao, hapana kulingana na kufananisha kati ya mafundisho yao na mafundisho ya Biblia.

Mbele ya yote—na kwa sasa hii ni jambo inayojulikana na watu wengi—masemo ya kwamba mafundisho yanapaswa kuchunguzwa na tunda yake tu ni yeye *mwenyewe* mafundisho. Tunapasa kwanza kuamua kama ile mafundisho ni kweli mbele ya kuwa na tumaini chochote kwa kuitumia kwa mafundisho mengine na wale wanayoyafundisha.

Musingi ya kibiblia kwa mafundisho haya inajulikana vizuri. Yesu yeye mwenyewe alisema ya kwamba tutajua manabi ya uwngo « kwa matunda yao … Muti muzuri haitazaa tunda mbaya, wala muti mubaya haitazaa tunda nzuri … Kwa hivi, mutawatambua kwa matunda yao » (Mat 7:15–20).

Sawa na majibu mawili ya mbele kwa kuchunguza mafundisho, hii inahusika sana na Biblia. Ni wazi, kama Yesu yeye mwenyewe alisema tunaweza kutambua manabi ya uwongo kwa matunda yao, hii ni njia ya haki kujaribu.

Shida ni ya kwamba watu wengine wanatumia njia hii kwa kuepuka uchunguzi ya mafundisho yao. Hata hivi, kuna mashairi mengine ndani ya Biblia yanayofundisha wakristo kuchunguza walimu wakristo (mufano, 1 Yoane 4:1–2). Kwa hivi Yesu hata maanisha ya kwamba mafundisho peke yake haitawezakuwa musingi kwa kuchunguza mutu anayejidai kuwa nabi. Ni vizuri kufahamu ya kwamba kuchunguza matunda ya utumishi ya mutu fulani ni njia moja nzuri ya kujaribu uhaki wake.

# Kuchunguza mafundisho ya musingi

Moja ya matunda mbaya ya mafundisho ya uwongo ni ya kwamba inagawa wakristo. Tena, hii si kosa ya wale wanachunguza mafundisho ya uwongo—ni kosa ya wale wanafundisha. Ni ya kushangaza kulaumu wale wanaopinga mafundisho ya uwongo!

Maneno mengine ya « tunda nzuri » toka watu wenye kufuata mafundisho mabaya ni pya ya kuchunguza. Kwa mufano, vikundi vingi ya dini (kama si yote) wanasema kwamba wafuasi yao wanapata mapendo sana, furaha na kutosheka. Shida hapa ni ya kwamba maneno haya yote haina uhaki ndani yake. Hakuna shaka ya kwamba watu wanaoishi pamoja katika kikundi lazima tu waone mapendo kati yao. Tafazali, fahamu ya kwamba sikatai ukweli ya kwamba ukristo wa kweli unatoa hali ya upeke kuhusu upendo. Hii ninasema ni ya kwamba mapendo, furaha na kutosheka yanaweza kuwa sehemu ya wasio wakristo kama jambo la kawaida, umutu na hii haingeweza kuchukuliwa kama faida ya milele ya kujua Yesu Kristo wa kweli.

Vivyo hivyo, vikundi vingine wanaoamini mafundisho ya uwongo wanasema ya kwamba imani yao inapasa kuwa kweli kwa sababu wameona miujiza katikati yao—zaidi sana uponyaji.

Bahati mbaya, Biblia ni wazi kabisa ikitoa angalisho kwetu ya kwamba waongozi ya dini wnaweza kufanya alama na miujiza ya uwongo (Mat 24:24; 2 Tes 2:9). Agano la Kale ilileta angalisho ya kwamba Mungu angeruhusu wakati ingine nabi ya uwongo kufanya alama ao mujiza kwa kuona kama watu walikuwa na hamu kuona sana katika miujiza ya kushangaza kuliko ndani ya Mungu wa kweli (Tor 15:1–5). Kwa hivi, hatutaweza kusema ya kwamba miujiza ni uhakika ya kwamba mafundisho ya mutu fulani inatoka kwa Mungu.

Kusema ya kwamba walimu wa uwongo wanaweza kufanya miujiza, sisemi kama miujiza yote inayohusika na mafundisho ya uwongo inatoka kwa shetani. Kila mara hatutaweza kusema kama miujiza ni ya kweli ao hapana. Miujiza ya uwongo zinaweza kufanywa na wachawi ao zinaweza kuwa uponyaji ya kweli. Inawezekana pya Mungu aponyeshe mutu yule aliyesikia mafundisho mabaya, lakini hakufahamu maana yake na imani yake ilikuwa ndani ya Mungu wa kweli na uwezo wake.
Si ya maana sana kila mara tuwe wenye kutoa hukumu kama haya. Ya lazima ni tusifanye kosa ya kufikili ya kwamba kila mujiza ni ukubali wa Mungu kwa mafundisho ya waongozi ya dini.



AC|FAR

Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Kuchunguza mafundisho ya musingi

## « Usitaje majina! »

Waongozi wakristo wengine wanataka kuruhusu mazungumuzo kuhusu mafundisho mengine ikiwa tu walimu ya mafundisho haya hawatajwe. Mafikili hapa ni ya kwamba kutokukubaliana na mafundisho fulani si magawanyiko, lakini kutaja mutu na kumuonyesha kama mwalimu ya uwongo ni magawanyiko.

Hii inamaanisha ya kwamba si vizuri « kugawa » kanisa kwa mambo ya mafundisho. Ikiwa mafundisho ni mubaya kabisa kwa kiwango kanisa kuikataa, hapo ni mubaya sana hadi wale wanaoendelea kuifundisha watajwe na kuonyeshwa wazi.

Mufano ya mutume Paulo ni ya maana. Kuna mara aliamua kutotaja majina ya walimu ya uwongo (mufano, 1 Tim 1:3). Kuna mara anataja majina yao. Kwa mufano, katika moja ya barua alitaja Himeneo na Alexanduro (1 Tim 1:10) na katika barua ingine alitaja tena Himeneo pamoja na Fileto (2 Tim 2:17). Inaonekana ya kwamba hakuna ubaya kutaja walimu ya uwongo.

Sababu moja kwa nini kuataja jina inaweza kuwa ya lazima ni ya kwamba kama mafundisho ya uwongo inazungumuziwa tu kwa jumla, watu watakana mara nyingi ya kwamba walimu wao ni wale wanafudisha uwongo. Mara nyingi watu hawataamini ya kwamba walimu wao wazuri wanatoa mafundisho ya uwongo isipokuwa masemo yao kamili kutolewa toka maandiko ao mahubiri yao.

Ikiwa mutu ni mwalimu ya uwongo yule hataweza kubadilika, tunahitaji kufanya zaidi kuliko tu kukataa mafundisho yake ya uwongo. Hakuna chochote tunaweza kufanya na yule mutu. « Mtu mzushi, nyuma ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili, umkatae; ukijua ya kuwa mtu kama huyo amegeuka mbali, naye amefanya zambi na amejihukumu mwenyewe. » (Tito 3:10–11). Haya ni maneno nguvu, hata makali, lakini yanatoka vile kwa Mungu. Mutu mwenye analeta magawanyiko kupitia mafundisho



tofauti, mafundisho ya uwongo yakukataliwa. Ili kukataa kwa mafundisho ichukue nafasi katika kanisa nzima, inahitaji kutaja mwalimu ya uwongo wazi.

Robert M. Bowman, Jr. • *Orthodoxy and Heresy* (Baker, 1992)

# Tutatafuta malaika kwa uongozi ya kiroho?

**Watu *wanaweza* kusema…**

Kuna watu wale wanasema tunapasa kutafuta malaika kutuambia kutuhusu, kuhusu Mungu, mbinguni, tutaishi namna gani na namna gani kupokea uponyaji na usaidizi. Vitabu vimeandikwa kama *Uliza malaika zako na Majibu toka malaika*. Wale wanaotafuta uongozi toka malaika wanawaita mara ingine « waongozi ya kiroho » ao hata *bachwezi* (Uganda).

**Lakini Bibia inasema…**

**Kwa kawaida malaika hawazungumuze na watu.**
Kwa kweli, hakuna mutu ndani ya Biblia aliyetafuta kuzungumuza na malaika ao aliyeambiwa kusikia toka malaika. Wakati malaika anapoonekana kwa watu ndani ya Biblia, inakuwa kama jambo la kushangaza kwa wengi. Maneno ya mwanzo ya malaika kwa mutu ni « Usiogope » ao « Usiwe na woga » (Mwanzo 21:17; Matayo 28:5; Luka 1:13, 30; 2:10).

Bahati mbaya, si malaika wote ao viumbe ya kiroho wanakuwa upande ya Mungu. Kuna kuwa na roho mbaya nyingi—pepo wachafu—wanaokuwa malaika walioanguka (Matayo 25:41). Hautaweza kuamini kila kitu unasikia toka malaika, zaidi sana hautaamini kila kitu unasikia toka watu. Jua ya kwamba shetani hana kitambulisho na jina « Shetani ». Anajifanya kama malaika ya nuru (2 Wakorinto 11:14).

Maandiko ni njia Mungu anatoa kweli yake kwa watu wake, kipimo kwa kujaribu kila dini (Matayo 22:29; Matendo 17:11; 2 Timoteo 3:16). Wakati malaika za Mungu wanapozungumuza kwa watu, hawapinge Biblia. Mutume Paulo analeta angalisho kwa wakristo kutokubali habari njema ingine, hata kama inaonekana kutoka kwa malaika ya mbinguni (Wagalatia 1:6–9).

Robert M. Bowman, Jr. • *10 Questions & Answers about Angels* (Rose Publishing, 2008)

## Unapasa vilie kujua …

Kutafuta habari toka malaika ina hatari ya kufungua njia kwa nguvu ya shetani. Kuona ya kwamba malaika hawana jibu wakati watu wanataka kuzungumuza nao, ikiwa dini yeyote inajibu, hii kweli haitoki kwa Mungu. Kupata ujumbe toka roho inaweza kuwa jambo la kufurahisha, lakini ni ya kudanganya, kwa sababu « sauti » kama ile si ile wanasema. Wengine wanatumia vitu ao njia ingine kwa kuficha habari ao kuchafua ukweli wa njia za kiroho, zaidi sana mazungumuzo na maroho. Mungu anakataa kabisa na anakataza mambo kama haya (Kumbukumbu la Torati 18:10–12).



AC|FAR

Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Tunaweza kutarajia malaika kututembelea?

**Watu *wanaweza* kusema…**

Malaika wanaonekana kwa watu kila wakati. Kulingana na mwandishi moja, « wale wanaotaka na wanakuwa tayari kuona malaika, wataona malaika ».

Waebrania 13:2, inayosema « Musisahau kuonyesha mapendo kwa wageni; maana kwa njia hii wengine wamekaribisha wageni; maana kwa njia hii wengine wamekaribisha malaika pasipo kujua », imechukuliwa kusema « sisi *sote* tumeona malaika kwa wakati fulani ya maisha yetu—pasipo kujua ».

**Lakini Bibia inasema…**

**Kuonekana kwa malaika ni ya maana na kwa jumla si ya kawaida.** AIjapokuwa Biblia inasema kuhusu kuonekana kwa malaika kwa watu, uchunguzi wa karibu uanonyesha ya kwamba kuonekana haya—hata kwa wakati ya Biblia—haikukuwa kila mara, jambo ya upeke na kama leo ilikuwa chache.

Malaika walionekana kwa watu kupasha habari ajabu ya kuzaliwa ya watu wakubwa (Isaka, Yoane Mubatizaji na Yesu), kuita manabi na waongozi wengine kwa utumishi (Isaya), kuleta ufunuo ya Mungu (Ezekieli, Yoane), kuokoa ao kuleta nguvu kwa manabi (Eliya, Elisha, Danieli) na mitume (Petro, Paulo), kutangaza ufufuko ya Yesu kwa wanawake kaburini na nyakati zingine. Mingi ya watu hawa waliona malaika mara moja tu katika maisha yao. Biblia haifundishe kama tunaweza kutarajia malaika kututembelea ao kuonekana kwa watu kila mara.

Jambo kubwa ya Waebrania 13:2 ni ya kwamba inatupasa kukaribisha wagenyi, si ya kwamba tunaweza kukutana na malaika. Inawezekana shairi inasema kuhusu Loti kukaribisha wagenyi waliobadilika kuwa malaika (Mwanzo 19). Kwa kweli, hakuna mutu alijua nani wagenyi wangegeuka kuwa, lakini si wazi wangekuwa malaika.

Ya maana sana, wakristo wangeshindana na jaribu ya kuweka nguvu yao na tumaini kukutana na malaika wakati hawana uhusiano ya nguvu, ya upeke na Mungu, *Muumbaji* ya kweli za malaika (1 Petro 1:8–12).

Robert M. Bowman, Jr. • *10 Questions & Answers about Angels* (Rose Publishing, 2008)



## Unapasa vilie kujua …

Mafikili ya kwamba watu wale wanakuwa na imani ya peke kwa utumishi ya malaika wanaweza kutambua ya kwamba kuona malaika haina musimamo yoyote ndani ya Biblia. Wapi malaika alionekana ndani ya Biblia, watu walioona malaika walishituka. Hakuna mara moja ndani ya Biblia mutu aliyetafuta kukutana na malaika. Hakuna vile mutu aliyeomba kwa kuona malaika ao aliyeonyesha hamu ya kumuona.

# U: Tutatambua uwezo na kazi za roho namna gani?

**J:** *Kwa **masemo**, **matendo** na **kuonekana**.*

Kwanza, **Shetani anazungumuza kupitia *masemo* yasiyoambatana na Andiko na zinaleta habari tunajua si ya kweli.** Hii ilitokea wakati Shetani alikaribia Eva na mara moja alipinga nini Mungu alimwambia (Mwanzo 3:4). Ilitokea wakati Yesu alikemea Petro kwa kukana angekufa, akisema: « Lakini akageuka, akamwambia Petro: Kwenda nyuma yangu, Shetani; kwani wewe ni jiwe la kukwaza kwangu kwani huwazi maneno yaliyo ya Mungu, lakini maneno yaliyo ya watu » (Matayo 16:23). Yesu alitambua ya kwamba nyuma ya sauti ya Petro kulikuwa roho ya Shetani. Kwa hivi, kila neno kuhusu Mungu ao inayoweza toka kwa Mungu inapaswa kuchunguzwa kulingana na Biblia.

Ya pili, **sawa Yesu alifanya miujiza, vivyo hivyo Shetani na malaika zake wanaweza kufanya alama na miujiza.** 2 Watesalonika 2:9 inaleta angalisho ya kwamba « kuja kwa yule mwenye uasi ni kwa mfano wa kutenda kwa Shetani na uwezo wote, na alama na ajabu ya uongo ». Katika siku za mwisho, Yesu anasema, « Kwa sababu makrosto ya uwongo watasimama, na manabii ya uwongo, nao wataonyesha alama kubwa na maajabu wapate kudanganya kama ikiwezekana, hata wachaguliwa » (Matayo 24:24). *Matendo*, hakuna shaka hata kama ni ya namna gani ao hata kama zinaonekana kuwa na faida, zinapaswa kuchunguzwa na kufananishwa na Neno la Mungu.

Ya tatu, **Shetani na maroho zake wanaweza pya kutambulikana katika *kuonekana*.** Shetani anashambulia wakristo kupitia walimu na waongozi wanaobadilisha ukweli. Watu kama wale wanaweza kila mara kuingiza mafundisho ile inakuwa kigeni kwa Andiko. Katika Matendo 16, Paulo na Sila walikutana na musichana mutumwa aliyekuwa na « roho ya kutabiri ». Aliwafuata muda ya siku nyingi, akisema: « Yule alifuata Paulo, na sisi, akapaza sauti, akilia: Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kutuhubiri njia ya wokovu » (Matendo 16:17). Ijapokuwa masemo yake yalikuwa kweli, roho nyuma yake ilikuwa uwongo na alitafuta kuvuta watu na ukweli ndogo akitafuta kutumia ile fasi kujaza mashitaki juu ya Habari Njema. Paulo alihukumu masemo yake, lakini alijua kwa kuonekana kwake ya kwamba roho zile zilimuongoza hazikukuwa kweli. Hakudanganywa na ile ingeonekana kama *kuonekana* ya utawa. Kwa hivi, kuonekana inapaswa kuchunguzwa vizuri sana na Maandiko.

Tim Challies • *The Discipline of Spiritual Discernment* (Crossway, 2007)



Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

AC|FAR

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Tofauti kati ya kanisa ya afya nzuri na sectes

- Kanisa ya afya nzuri inaweka mkazo juu ya Andiko (2 Tim 3:16–17). *Mara nyingi sectes zinaweka mkazo juu ya mamlaka ya waongozi wanaosema walipokea ujumbe ingine toka kwa Mungu.*
- Kanisa ya afya nzuri inaongozwa na watu wanayoongoza kupitia mufano nguvu lakini ya upole, mashauri na kutia moyo (2 Tim 2:24–25; 1 Pet 5:1–3). *Waongozi za sectes mara nyingi wanatawala na nguvu na kuogopesha, na sheria na woga.*
- Kanisa ya afya nzuri inafundisha uhusiano ya utawa na jamii (1 Kor 5:9–11; 1 Pet 2:11–17). *Sectes zingine zinalazimisha watu kutoka kabisa toka jamii ila tu kwa kupata pesa.*
- Kanisa ya afya nzuri inatia moyo kwa upendo na heshima kwa jamaa ya wanamemba, wakitambua ya kwamba kuzarau jamaa ya mwanemba inaweza kusababisha magawanyiko (Mat 10:34–37; Efe 5:22—6:4). *Sectes zinaweza kuweka mkazo kuzarau asiyekuwa mwanamemba pasipo kujali nini wazazi wake wanafikili kuhusu Krsito.*
- Kanisa ya afya nzuri inachunga mkazo juu ya Krsito (1 Kor 1:10–17; 2 Kor 4:5–6). *Sectes mara nyingi zinageuza ile mkazo juu ya mutu na mafundisho ya waongozi yao.*
- Kanisa ya afya nzuri nianaonyesha heshima hata kwa watu na shirika wanafikili zinakuwa chini ya nguvu ya Shetani (Rom 13:1; Tito 3:1; 1 Pet 2:13–17). *Sectes mara nyingi zinatia moyo kuzarau na kukosa heshima kwa watu wa inje.*
- Kanisa ya afya nzuri inatumika katika ukamilifu kabisa (2 Kor 4:2). *Sectes mara nyingi zinatumika na sheria ya kwamba kila kitu kinacholinda na kuendelesha kundi ni nzuri.*
- Kanisa ya afya nzuri inalazimisha waongozi yao kuwa na mwenendo nzuri na utakaso (1 Tim 3:1; Tito 1:5–9). *Sectes mara nyingi zinaruhusu waongozi yao kuishi « juu ya sheria ».*
- Kanisa ya afya nzuri inafundisha ya kwamba kutoa inapasa kuwa kutaka kwa moyo (2 Kor 9:7). *Sectes mara nyingi zinatangaza wazi sheria ya kutoa ao zinaomba nyumba na vitu vitolewe kwa kundi.*
- Kanisa ya afya nzuri inatia moyo wanamemba kuamua wao wenyewe kama wanaongozwa kulingana na Biblia (Efe 4:11–16; 1 Yoane 4:1–6). *Sectes mara nyingi zinakata moyo ao zinakataza uchunguzi yoyote.*
- Kanisa ya afya nzuri inatambua na inakubali wote wale wanakiri jina la Kristo katika imani na matendo (1 Kor 3:1–9; Fil 1:15–18; 2 Yoane 7–11). *Sectes mara nyingi zinatambua tu wanamemba yao.*
- Kanisa ya afya nzuri inafundisha njia za Biblia, zinazosababisha kukomaa ya upeke, mafikili, uamuzi na kuwa mutu muzima (2 Tim 3:16–17; 1 Pet 2:1–3). *Sectes mara nyigi zinaweka hali ya kutawaliwa, inayofanyiza mwongozi kuchukua uamuzi yote ya maana.*

# Tofauti kati ya kanisa ya afya nzuri na sectes

- Kanisa ya afya nzuri inaepuka kucheza na mafikili, ikiamini katika uwezo wa Roho ya Mungu kutumika ndani ya maisha ya watu kupitia Neno la Mungu (1 Kor 2:3–5; 2 Kor 2:17; 101–6). *Sectes mara nyingi zinatumia njia ya kubadilisha mwenendo zilizotumiwa kwa wale waliokuwa katika gereza ya vita.*
- Kanisa ya afya nzuri inapendwa ao inachukiwa kwa sababu ya kufananishwa kwao na Kristo na Neno lake (Mat 5:11; Yoane 15:18–21). *Sectes mara nyingi zinapendwa ao zinachukiwa kwa sababu ile wanaongeza ao wanapunguza toka Kristo na Neno lake.*

## Tabia za kuumiza!

Wakati sisi sote tunahitaji kutafuta mafikili ya hatari ndani yetu sisi wenyewe, tabia zingine mara nyingi zinaonekana katika sectes. Zinakuwa:

- Kuwa chini ya waongozi wanaokuwa na zawadi, wakisema wanazungumuza kwa jina ya Mungu wanajiweka juu ya kila kitu.
- Uongozi mbaya kupita kipimo, kujichafua na unafiki ya dini za desturi.
- Kujiondoa toka jamii, kwa imani ya kwamba « sisi tu » tunatoa zabihu za kufaa kwa Mungu.
- Kukata njia zote za inje kwa kupata habari.
- Kweli inabadilika kutoka kwa ile ya uaminfu kwa ile inakuwa na faida kwa kikundi
- Kujihesabia haki kulingana na imani ya kwamba watu wa inje wanakuwa chini ya uongozi ya Shetani.
- Kupoteza uhuru kama mafikili ya upeke, kujisikia na uchaguzi zinabadilishwa na mafikili ya kundi, kujisikia kwao na uamuzi.
- Kupoteza zamiri, kundi na waongozi wake wakikokota mwanamemba katika tabia (zaidi ya uasherati) zinazoharibu hali nzuri.
- Kusimamisha mafikili toka ile iliyoahidiwa kwa ile imepokelewa.
- Woga ya kuacha kundi kwa kupoteza uzima wa milele na zawabu.

*How to Identify a Dangerous Religious Group* (RBC Ministries, 2002)



Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
ACFAR
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Nani ana imani?



Kwanza, Mungu hana imani. Biblia hasemi kamwe ya kwamba Mungu ana imani. Imani inaweka mutu kuweka tumaini ndani ya mutu mwengine ao kitu; ni kutawaliwa na mutu mwengine ao kitu. Mutu anaweza kutumia neno « imani » akifikilia Mungu  kwa kuwa Mungu anatosheka na uwezo na hekima wake yeye mwenyewe. Mungu anajua nini anafanya!

Lakini hii si ile walimu wa Neno-Imani wanamaanisha kwa imani. Wanapotumia, imani ni uwezo ao nguvu inayotumika kulingana na sheria za kiroho zisizobadilika kupitia maneno yaliyosemwa kwa kutimiza ile mutu anayezungumuza anaamini na anataka. Kulinganana na waalimu wa Neno-Imani, nguvu ao uwezo ule ya imani ni ile kitu Mungu anakuwa nayo na hata sisi tunaweza kuwa nayo. Lakini Biblia haisemi kitu kuhusu mafikili ile.

---

Ya kufuata, tunapasa kuweka mukazo ya kwamba *wakristo wana imani ya kuokoa, lakini si lazima imani ya kufanya miujiza*. Kwa kweli imani ni zawadi ya Mungu, ginsi walimu ya Neno-Imani wanavyosema (Rom. 12:3; Efe. 2:8). Lakini Mungu hakuleta « imani ya kuhamisha kilima » kwa kila mukristo. Paulo anataja imani kama ile katika zawadi za Roho (1 Kor. 12:9; 13:2; ona Rom. 12:3, 6), na anaendelea kuonyesha wazi ya kwamba wakristo wote hawana zawadi ya aina moja (Rom. 12:4–6; 1 Kor. 12:4–6, 14–19, 29–30).

Yesu alipozungumuzia kuhusu imani ya kuhamisha milima (Mat. 21:21; Marko 11:23), hakuamanisha ya kwamba kila mutu angeweza kuwa na imani ya namna ile. Maoni yake ilikuwa kila mutu aliyekuwa na imani ya namna ile angepata ile aliamini. Lakini imani kama ile inatoka tu kutoka kwa Mungu na tu ginsi yeye peke yake anataka (1 Kor. 12:11).

Ninakubali ya kwamba kuna mara Mungu anamupatia mukristo uhakika isiyo ya kawaida ya kwamba anataka kufanya jambo fulani inayokuwa nguvu kwa mwanadamu kuamini. Lakini Yesu hakusema ya kwamba Mungu angefanya ile kwa kila mukristo ao ya kwamba ile ingekuwa njia ya kawaida kwa maisha ya kila mukristo.

## Nani ana imani?

Wakristo kama watu wasioamini. Hii ni kwa sababu imani si kitu kila mutu anakuwa naye, lakini anashindwa kuitumizia; bali, ni tumaini inayotolewa na Mungu ndani ya Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana.

### Imani ni nini?

Imani haizungumuziwe katika Andiko kama « nguvu » ao uwezo ingine. Mafikili katika mafundisho ya Neno-Imani ni ya kwamba wanadamu wanaweza, wakitumia imani, kufanyiza ile isiyo kweli kuwa kweli ao ya kiroho kuonekana kimwili, inapinga Andiko. Acha nilete mufano nikitumia maandiko yaliyotumiwa na walimu ya Neno-Imani kwa kusimamisha mafikili yao juu ya imani.

Walimu ya Neno-Imani wanataja mara nyingi Waroma 4:17 na wanasema ya kwamba wakristo wangepasa kutafuta kuiga neno Mungu aliumba naye. Lakini, ukweli ni ya kwamba hii andiko inaonyesha Mungu kama wa peke anayeweza fanya ile isiyokuwa iwe (Rom 4:17). Paulo anasema wazi ya kwamba Abrahamu aliamini *Mungu* kwa sababu *ni* Mungu (*hapana* Abrahamu) ndiye alikuwa na uwezo ya kuleta uzima kwa aliyekufa na kufanyiza ile haikukuwa iwe. Ni Mungu aliyeiahidi na ni Mungu peke yake alikuwa na uwezo kuitimiza (shairi 20–21).

Waefeso 1:3 inatajwa mara ingine kuhakikisha ya kwamba wakristo wana afya na kuendelea inayowaongoja katika hali ya kiroho, ikihitaji tu kukiri kwa imani ili itimilike. Hii ni njia ya kushangaza sana ya kutokufahamu Andiko hata kuliko mufano tulitoa mbele. Baraka za kiroho ile Paulo anasema tunapata ndani ya Kristo (Efe 1:3) ni kufanywa wana (shairi 5), ukombozi na usamehe (shairi 7), kujua mapenzi yake (shairi 9), hali ya wariti (shairi 11) na kukaa ya Roho ndani yetu (shairi 13). Hii si baraka za kuonekana ya afya kimwili ao kupata pesa zinazongoja kuhamishwa kwa nguvu ya imani kutoka isiyoonekana kwa inayoonekana.

Hali moja ya kuharibu sana ya mafundisho ya Neno-Imani ni mafundisho yake ya kwamba imani ya kweli inaweza kuwa tofauti na hali za kweli ao akili. Sasa, kuna mbegu ya kweli ndani ya ile mafundisho. Tunapasa kuamini Mungu, haijalisi hata kama kuna nini. Lakini imani *haisahau* mambo yanayooenekana. Zaidi, imani inakataa kuruhusu yale yanayoonekana kutingiza tumaini yetu katika uwezo ya Mungu kutimiza ile aliahidi.


Angalia tena mafundisho ya Paulo kuhusu Abrahamu katika Waroma 4. Abrahamu hakukataa ao kusahau ya kwamba mwii wake ilkuwa muzee sana kwa kuzaa. Abrahamu « hakukiri » ya



ACFAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

kwamba, ijapokuwa kuonekana kwake na ginsi alikuwa akijisikia, alikuwa kabisa mwanaume wa nguvu! Bali, alikiri ya kwamba Mungu angeweza kuleta uzima mpya toka mwili wake, ijapokuwa ilikuwa kama imekufa (Rom 4:19).

Walimu ya Neno-Imani wanajua sana kutaja masemo ya Paulo « Kwa sababu hatuangalii vitu vinavyoonekana; lakini vitu visivyoonekana. » (2 Kor 4:18a). Lakini kueleza maneno ya Paulo hapa kama sheria ya kukataa ukweli ya ile inaoneka ni kuchukua masemo ya mutu inje ya pahali (contexte) ndani yake aliitumia. Paulo anaenda mara moja kuonyesha kwa sababu gani « hakuona ile » inaonekana, lakini ile isiyoonekana: « kwa sababu vitu vinavyoonekana ni vya saa kidogo tu lakini vitu visivyoonekana ni vya milele » (shairi 18b). Paulo anaposema « hakuona » kwa vitu anavyoona, anazungumuza kwa fumbo—kwa kuwa mutu hataweza kuona kitu fulani asipoiangalia!




Paulo anamaanisha ya kwamba haishi maisha yake kulingana tu na ile anaweza kuona ao kuruhusu mambo ya karibu, ya muda kumupeleka mbali kwa kutimiza mwito wa Mungu kwa maisha yake. Pasipo na kukataa ukweli ya muda na ya kuonekana, Paulo anazitambua kabisa. Ona ile alisema katika mashairi mbili juu ya kwamba « mutu wa inje... » (shairi 16). Hii ni ile walimu ya Neno-Imani wanaweaita « kukiri ya mubaya »; ni kukubali wazi ya kwamba mwili inaharibika na kuanguka. Kwa kweli, hakuna shida kusema maneno kama haya.

Kutembea kwa imani, hapana kwa kuona (2 Kor 5:7), haimaanishe kukataa ukweli ya ile tunaona. Bali, ni kuamini Mungu kutupigania na baraka zake ijapokuwa hali ngumu ya maisha haiko kila mara ile tungetaka iwe. Inamaanisha kuishi ndani ya tumaini ya kwamba Mungu atatimiza ahadi yake ya kutupatia uzima isiyo na mwisho katika ufufuko (shairi 1–8).

Ni pya kosa kusema ya kwamba imani itakuwa mbali na akili. Imani haikose akili kamwe, kwa sababu ni hali ya tumaini ndani ya Mungu aliyeumba kila kitu na anayeongoza dunia katika kweli. Bali, imani inakataa kutegemea tu ile akili inaweza kutambua. « Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, Wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe » (Mez 3:5) haimaanishe « kufikili na akili ». Ila, inamaanisha kuishi kama unaweza kuongoza maisha yako binafsi mbali na hekima ya kujua na kuogopa Mungu (fananisha shairi 6–7).

Robert M. Bowman, Jr. • *The Word-Faith Controversy* (unabridged)


# Wahubiri ya imani na Biblia

Hapa kuna sehemu tatu ya Maandiko yale walimu ya Neno-Imani wanatumia vibaya wakati wanaposema ya kwamba Mungu anahakikisaha afya na mali kwa watu wake kama wanasema maneno ya imani.

## « Ishi siku nyingi na uendelee »
(3 Yoane 2)

Moja ya maandiko yale ni maombi ya Yoane kwa rafiki yake Gayo « Mupenzi, ninaomba usitawi katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako inavyositawi » (3 Yoane 2). Hakuna jambo mbaya kuombea watu waendelee na wapate mali. Lakini, inafaa kutambua ya kwamba Yoane hasemi maombi yake itapata jibu mara moja. Yoane anaombea mutu mwengine, hapana yeye mwenyewe. Hata kwa misingi ya Neno-Imani—ao hakose sana kwa Neno-Imani misingi—ni ngumu kuona namna gani maombi ya Yoane ingeweza kuhakikisha afya na mali ya Gayo.

Hakika, kuona kwamba Yoane aliomba namna hii inaonyesha ya kwamba aliamini afya na mali ya Gayo zinaangalia Mungu, hapana Gayo! Yoane hakuambia Gayo kuuliza afya na mali.



## « Baraka mara mia »
(Marko 10:29–30)

Shairi ile walimu wanaweka mukazo juu yake kuhusu pesa ni Marko 10:29–30. Katika shairi hii Yesu anaambia wanafunzi wake Yesu akasema:

> « Kweli ninawaambia ninyi, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu na kwa ajili ya Habari Njema, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na mateso, na katika ulimwengu unaokuja uzima wa milele ».

Hakika, Yesu hakumaanisha kama unaacha nyumba yako na kumufuata, utapata, ginsi inavyoandikwa, nyumba mia; ao ikiwa mutu atafuata Kristo atapata wamama mia! Ile Yesu anasema ni neno kama hii: Ikiwa itawezekana kuacha nyuma mali ao ndugu ya damu kufuata Kristo (ginsi ilivyokuwa kwa wanafunzi kumi na mbili



ACFAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism

Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

na ginsi inavyokuwa mara ingine kwa wafuasi wake leo), mwamini mwenye anafanya hivyo atajikuta sehemu ya « jamaa » kubwa. Hii jamaa ni kanisa, na watu wa kanisa watakuwa kwake ndugu, dada, mama, baba na watoto, na wale watamufungulia milango ya nyumba zao, kumukulisha toka shamba zao. Hii ni maisha ya wainjilisti waaminifu na wamisionari toka inchi za kigeni kwa muda ya miaka mingi.

## Mungu ni muponyaji
(Zaburi 103:2–3; 107:20)

Ya kufuata, acha tuone mashairi mawili toka Zaburi. Katika Zaburi 103:2–3 Daudi anajikumbusha ya kwamba Mungu ni mwenye kusamehe zambi zake zote na kuponya magonjwa yake yote. Si wazi kabisa kama hii ni ahadi ya kwamba Mungu ataponya magonjwa yote ya waamini wakati wowote ya historia. Katika shairi la kufuata Daudi anajikumbusha « Anayekomboa uzima wako toka shimoni; Anayekutia taji ya wema na rehema » (shairi 4), lakini hii si uhakika ya kwamba Mungu hataruhusu Daudi akufe. Tena, bila shaka Mungu « ataponya » waamini wote na kila ugonjwa ao kilema akiwafufua toka mauti katika miili ya kukamilika. Tukiongojea ile, kila uponyaji tunapata, ikiwa kwa njia ya kawaida ao ya ajabu, ni baraka toka kwa Mungu.

Katika Zaburi 107:20 kuna jambo lingine tofauti kabisa. Mwandishi ya Zaburi anazungumuza kuhusu watu walioasi Mungu na « waliopata mateso kwa sababu ya zambi zao » (shairi 18). Na wakalia kwa Mungu na aliwaokoa toka kifo ya karibu (shairi 19). Hakuna ahadi ya jumla hapa kwa uponyaji kimwili kwa kila mutu kulingana na hali anakuwa ndani yake.

## Uvumilivu ya Yobu
(Yakobo 5:10–11)

Neno-Imani inasema ya kwamba watu wanaoishi kwa imani wanawezapata « mateso », lakini « magonjwa » haiambatane na sehemu ya Yobu, kwa sababu ugonjwa wake ulikuwa sehemu kubwa ya « mateso » yake (shairi 10–11). Waalimu wengi ya Neno-Imani wanasema Yobu alikuwa mufano ya *kutokuamini*, lakini Yakobo hakubali hivi. Ila, Yobu ni mufano wa uvumilivu (shairi 11) inayoonyesha *imani ya kweli* (fananisha Yakobo 1:3–4).

Kisha Yobu kusema, « Bwana anatoa na Bwana anatwaa » (Yobu 1:21–22; 2:10). Masemo ya kwamba Yobu alijifikishia mateso yeye mwenyewe kwa sababu ya « kukiri ya mubaya » ni uwongo.

Ni kweli ya kwamba *kisha* rafiki zake walijaribu kueleza mateso yake, Yobu alijiona mwenye haki na ilibidi atubu (40:3–5; 42:1–6). Lakini hapo Mungu aliambia rafiki za Yobu ya kwamba hawakumuzungumuzia maneno ya haki, sawa Yobu alivyiofanya (42:7). Kwa sababu rafiki za Yobu walisema ya kwamba Yobu alijiletea mateso kwa sababu ya zambi zake, tena mafikili hii ilionekana si ya kweli.

Robert M. Bowman, Jr. • *The Word-Faith Controversy* (unabridged)

# Mezali kuhusu pesa

| | |
|---|---|
| **Rushwa** | Mwenye kutamani faida anataabisha nyumba yake mwenyewe; Lakini mwenye kuchukia zawadi ataishi.—MEZALI 15:27<br>Mtu mwovu anatoa awadi kifuani, Ili kuipotosha njia za hukumu.—MEZALI 17:23 |
| **Deni** | Usiwe mmoja wao wanaopiga mikono; Au wa wale walio zamana kwa deni za watu; Kama huna kitu cha kulipa, kwa nini atatoa kitanda chako chini yako? —MEZALI 22:26–27 |
| **Uangalifu** | Yeye anayetenda kwa mkono mlegevu anageuka kuwa maskini; Lakini mkono wake aliye na bidii unatajirisha hekima. Mwenye kukusanya kwa wakati wa hari ni mwana mwenye hekima; Lakini yeye anayelala wakati wa mavuno ni mwana anayepatisha haya —MEZALI 10:4–5 |
| **Tama** | Moyo ulio mzima ni uzima wa mwili; Lakini wivu ni kuoza kwa wa mifupa. —MEZALI 14:30 |
| **Wizi** | Chakula cha udanganyifu ni kitamu kwa mtu; Lakini nyuma kinywa chake kitajazwa mawe madogo. —MEZALI 20:17 |
| **Ukarimu** | Yeye anayehurumia maskini anakopa kwa Bwana; Naye atamlipa kwa tendo lake zuri. —MEZALI 19:17 |
| **Kukusanya vitu** | Yeye anayenyima nafaka, watu watamtukana; Lakini baraka itakuwa kwa kichwa chake anaiuza. —MEZALI 11:26 |
| **Usawa katika biashara** | Mwovu anapata mshahara wa udanganyifu; Lakini mwenye kupanda haki ana zawabu ya hakika. —MEZALI 11:18 |
| **Kiasi** | Usijitaabishe ili kupata utajiri; Acha kutegemea hekima yao mwenyewe. —MEZALI 23:4 |
| **Uvumilivu** | Utajiri unaoopatikana kwa haraka utapunguka; Lakini mwenye kukusanya kwa njia ya kazi atazidishiwa. —MEZALI 13:11 |
| **Ushuhuda** | Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi; Na ukubali kuliko feza na zahabu. —MEZALI 22:1 |
| **Kutokujizuiza** | Mwenye husuda afanya haraka kuwa tajiri; Wala haufikiri uhitaji utakaomjilia. —MEZALI 28:22 |
| **Kufaulu** | Mwenye kutumainia mali zake ataanguka; Lakini mwenye haki atasitawi kama majani mabichi. —MEZALI 11:28 |
| **Mali ya haki** | Si afazali kupata hekima kuliko zahabu? Ndiyo, inafaa kuchagua ufahamu kuliko feza. —MEZALI 16:16 |
| **Kazi** | Mwenye kulima shamba lake atakuwa na chakula tele; Lakini mwenye kufuata mambo bule anakosa ufahamu. —MEZALI 12:11 |

Jessica Curiel • *What the Bible Says About Money* (Rose Publishing, 2009)



ACFAR
Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism
Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Tumainia Mungu, hapana pesa



Ahadi za uwongo ya pesa ni za kuchezacheza na hazitosheke. Ahadi za Mungu ni milele na kila mara ya kutumainia.

| | |
|---|---|
| **Usalama** | Uwaagize walio matajiri katika ulimwengu huu matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri unaotoweka upesi, lakini Mungu aliye hai, anayetupa sisi vitu vyote ili tufurahie navyo. —1 TIMOTEO 6:17 |
| **Uwezo** | Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifazaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakuletea nguvu, ndiyo nitakusaidia, ndiyo nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu. Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitashika mkono wako wa kuume, nikikuambia: Usiogope; nitakusaidia. —ISAYA 41:10, 13 |
| **Faida na kusimama wataketi katika jamii** | Na watakuja watu toka mashariki na magaribi, na toka kaskazini na kusini, nao ufalme wa Mungu. Na tazama, walio wa mwisho watakuwa wa kwanza, na walio wa kwanza watakuwa wa mwisho. —LUKA 13:29–30 |
| **Kufaulu** | Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni, Mungu hakuchagua masikini za dunia wawe matajiri ya imani na wariti wa ufalme ambao aliwaahidia ambao wanampenda? —YAKOBO 2:5 |
| **Mapendo na kuvuta angalisho** | Bwana, Mungu wako, ni katikati yako mwenye uwezo kuokoa; atafurahi juu yako kwa furaha kuu, atapumzika katika upendo yake, atakufurahi juu yako na kwa kuimba. —ZEFANIA 3:17 |
| **Salama ya mafikili** | Kujeni kwangu, ninyi wote munaosumbukao na wenye mzigo na mizito, nami nitawapumzisha ninyi. —MATAYO 11:28 |
| **Uhuru toka matokeo** | Mali hazina faida kwa siku ya gazabu; Lakini haki inaokoa na mauti. —MEZALI 11:4 |
| **Furaha** | Ujifurahishe vivlvile ndani ya Bwana, Naye atakupa wewe maombi ya moyo wako. —ZABURI 37:4 |



Muwe wafungulifu kwa mapendo ya feza: muwe razi na vitu mulivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe alisema:

« Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha hata kidogo. »

—WAEBRANIA 13:5

Jessica Curiel • *What the Bible Says About Money* (Rose Publishing, 2009)

# Ya kufanya na ya kutokufanya na pesa



| Ya kutokufanya | Ya kufanya |
|---|---|
| Usiipenda! LUKA 16:13 | Penda Mungu. TORATI 6:5 |
| Usifikili itadumu. YEREMIA 17:11 | Ila tu vitu vya Mungu vitadumu. MATAYO 19:21 |
| Usifikili inaweza kukuokoa. ZABURI 37:16–17 | Kumbuka ni Mungu peke anaweza kukuokoa. ZABURI 27:1 |
| Usiitumikie. MATAYO 6:24 | Tumikia Mungu. 1 PETRO 5:2; MARKO 12:41–44 |
| Usitamani wengine wala wanakuwa naye. KUTOKA 20:17 | Ufurahie ile unakuwa nayo. LUKA 3:14 |
| Usiikusanye. YAKOBO 5:3–6 | Kumbuka Mungu analeta. YOBU 1:20–21; YAKOBO 4:13–15 |
| Usiwe mupumbafu naye. MEZALI 17:16 | Uitumie kwa hekima. MEZALI 31:10–31 |
| Usifikili inaweza kuchukua fasi ya shida. MEZALI 15:16–17 | Pata salama ndani ya Mungu. WAROMA 15:13 |
| Usiitegemee. ZABURI 62:10 | Tegemea Bwana. MEZALI 18:10–11 |
| Usifikili inaweza kununua Baraka za Mungu. MATENDO 8:9–24 | Pata baraka ukiishi kwa Mungu. 2 WAKORINTO 6:10 |
| Usiitumie kwa wizi. MIKA 2:2 | Lipa deni zako naye. ZABURI 37:21 |
| Usitese watu kwa kuipata. MEZALI 22:16; AMOSI 2:6–7 | Tumika kwa kuipata. 2 WATESALONIKA 3:9–11 |
| Usiibe. TITO 2:6–7; KUTOKA 20:15 | Uichunge katika haki. WALAWI 25:14; ZABURI 112:5 |
| Usiheshimie sana wala wanakuwa naye. YAK 2:2–6 | Uitoe kwa wale katika hitaji. MATAYO 5:41–42 |
| Usiitumie pasipo uaminifu. MEZALI 13:11 | Uwe mwaminfu kuitumia. MEZALI 11:1 |
| Usiitumie kwa ubaya. EZEKIELI 8:12–13 | Heshimu Mungu naye. MEZALI 3:9–10 |
| Usiinyanganye. EZEKIELI 22:29 | Uipate kwa haki. MEZALI 13:4 |
| Usiitamani. LUKA 22:29 | Uitoe ukijua. 1 WAKORINTO 16:2 |
| Usiogope kwa ajili yake. MATAYO 6:34 | Jua ya kwamba Mungu atakushurulikia. MEZALI 15:25 |

Jessica Curiel • *What the Bible Says About Money* (Rose Publishing, 2009)




ACFAR

Equipping God's People across Borders and Cultures
for Discernment, the Defence of the Faith, and Cult Evangelism


Post Office Box 72405—Clock Tower, Kampala, UGANDA
www.ACFAR.org • e-mail info@ACFAR.org • tel. +256782 000 664 • office +256713 000 664

# Helpful Books on False Teachings and Related Topics in Africa

*Africa Bible Commentary*. Nairobi: WordAlive Publishers, 2006; 1,616 pages




(Includes helpful articles on the Bible's view of Angels, Demons and Powers; Dreams; Faith and the Search for Signs; Funeral and Burial Rites; Initiation Rites; Idolatry; Prophets and Apostles; Syncretism; Taboos; The Bible and Polygamy; Theological Heresy; The Place of Traditional Sacrifices; The Role of the Ancestors; Witchcraft; and Yahweh and Other Gods.)






Femi Adeleye, *The Preachers of a Different Gospel: A Pilgrim's Reflections on Contemporary Trends in Christianity*. Nairobi: WordAlive Publishers, 2011; 160 pages




Marvin S. Wolford, *Free Indeed from Sorcery Bondage*. San Rafael, CA: Pathway Press, 1999; 258 pages

Richard J. Gehman, *Who Are the Living-Dead? A Theology of Death, Life After Death and the Living-Dead*. Nairobi: Evangel Publishing House, 1999; 350 pages






Richard J. Gehman, *African Traditional Religion in Biblical Perspective*. Nairobi: East African Educational Publishers, 1994, 2005 (revised edition); 314 pages

Yusufu Turaki, *Foundations of African Traditional Religion and Worldview*. Nairobi: WordAlive Publishers, 2006; 128 pages



**Note:** *By including a work we are not necessarily endorsing of all its contents or of other works by the same author or publisher.*

# Helpful Web Sites on Cultic Groups and Christian Discernment



**Apologetics Index**
www.apologeticsindex.com

**Institute for Religious Research**
www.irr.org

**Stand to Reason**
www.str.org

**Centers for Apologetics Research**
www.TheCenters.org

**Watchman Fellowship**
www.watchman.org

**Mormonism Research Ministry**
www.mrm.org

**Christian Answers for the New Age**
www.christiananswersforthenewage.org

**Life Assurance Ministries**
www.lifeassuranceministries.org

**Note:** *By including a web site we are not necessarily endorsing all its contents or other materials by the same author(s) or organization.*

# THIS NOTEBOOK IS NOT TO BE SOLD

Shukuru Mungu kwa sababu kuna watu kwa kanisa ya leo wanaojitoa kabisa kupigania na kushika ukweli wa Mungu uliyofunuliwa. Lakina, mara nyingine wanashindwa kabisa kupenda. Wanapofikila wananusa mafundisho mbaya, pua yao inaanza kuwasha, mishipa yao zinasimama na nuru ya vota inaingia ndani ya macho yao. Hakuna kitu kingine wanafurahi isipokuwa tu vita. Wnegine wanfanya kosa tofauti. Wanajitoa kabisa kushika na kuonyesha upendo ya ndugu, lakini wakifanya hivyo wanajitayarisha hata kutoa mambo ya kweli ya ufunuo. Hali hizi zote zinakosa usawa na si ya kibiblia. Ukweli unakuwa nguvu kama hairegezwe na upendo; mapendo inakuwa teketeke kama haitiwi nguvu na ukweli. Mutume [Paulo] anatuita kushika zote mbili pamoja, jambo halitakuwa ngumu kwa waamini wanaojazwa Roho Mutakatifu 'Roho y akweli,' na tunda lake la kwanza ni 'upendo.' Hakuna njia ingine kama hii kwa umoja ya kutosha ya kikristo.

— John R.W. Stott | *Vers une nouvelle société* (Grâce et Vérité, 2010)

Brought to you by

**Africa Centre for Apologetics Research**

Post Office Box 72405
Clocktower, Kampala, UGANDA

**Coordinator:** +256 706 100 664
**Administrator:** +256 753 537 190
**Office:** +256 706 378 254
**Email:** info@acfar.org
**Web site:** www.acfar.org

« Na hii ndiyo ninayoomba, hata mapendo yenu yazidi kuongezeka mengi sana katika hekima na ufahamu wote; ili mupate kukubali maneno yaliyo mema; ili muwe na moyo safi, pasipo kosa, mupaka siku ya Kristo; mukijazwa matunda y ahaki yaliyo kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu. »

(Wafilipi 1:9–11)

« ...mutembee kama watoto wa nuru (kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli), mukijaribu nini inayopendeza Bwana. »

(Waefeso 5:8b–10)

« Na musifananishwe kwa namna ya dunia hii; lakini mugeuzwe kwa kufanya upya nia zenu, mupate kujua sana mapenzi ya Mungu, yaliyo mema, ya kumupendeza, na ukamilifu. »

(Waroma 12:2)

REV4 11/15